# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Agosti 4, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581758

www.ippmedia.com

www.facebook.com/nipashetz

www.twitter.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Álvarez kuamua hatima yake Man City**

UKURASA 22

**TPA** yatoa ufafanuzi madai ya rushwa

UKURASA WA 2



**CCM** yaita wanachama kugombea ubunge EALA

UKURASA WA 3



**Wivu** wa mke unavyochangia mume kufariki kabla ya wakati

UKURASA WA 11

RIPOTI MAALUM

# Mahubiri ndani ya mabasi yalivyogeuka kero kwa abiria

UKURASA 4





Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akimsikiliza mmoja wa wafugaji wa asili aliyeanza kufuga ng'ombe kisasa katika kampeni ya Tutunzane Mvomero, baada ya kuizindua mkoani Morogoro jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 2

## Mwabukusi atema cheche baada ya kula kiapo



# Rais Samia achoshwa matamko ya viongozi, ataka wawe wabunifu

UK. 3

**MICHEZO** GAMONDI AWAITA MASHABIKI KWA MKAPA UK.24

**MAONI,** UK.6

# TPA yatoa ufafanuzi madai ya rushwa

**Na Adela Madyane**, KIGOMA

BAADA ya malalamiko ya baadhi ya wafanyabiashara kuhusu tozo na utaratibu wa ukusanyaji mapato Bandari za Kigoma kuwa chanzo kikuu cha mianya ya rushwa ambayo huleta hasara kwa serikali, Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Edward Mabula, ametoa ufafanuzi kwamba hakuna upotevu wowote.

Jumatano ya wiki hii, katika kikao cha Baraza la Biashara la Mkoa kilichofanyika ukumbi wa Lake Tanganyika, mkoani hapa, baadhi ya wajumbe walilalamikia utaratibu wa ukusanyaji wa mapato katika Bandari ya Kibirizi iliyoko Manispaa ya Kigoma Ujiji, kuwa chanzo kikuu cha mianya ya rushwa ambayo huisababishia hasara serikali.

Walisema makusanyo mengi ya tozo hayaingii serikalini kwa kuwa yanatozwa holela bila mpangilio maalum.

Akizungumza jana na mwandishi wa habari hii kuhusu malalamiko hayo, Mabula alisema kimsingi hoja iliyowasilishwa katika baraza hilo ilihusu kuondolewa kwa tozo ya bandari ya Dola 10 ambayo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) haitozi.

"TPA haina tozo ya Dola za Kimarekani 10 wala Dola tano. Malalamiko ya Dola 25 hadi 30 yanaashiria kuwa mteja wa aina hiyo anakuwa amekutwa na ukiukwaji wa taratibu za sheria na hivyo hulipa kama hongo ili kuepuka adhabu na huo sio utaratibu," alisema.

Mabula alisema malipo yote hutolewa risiti halali na iwapo kuna yanayofanyika bila risiti halali, mteja anasisitizwa kutoa taarifa katika mamlaka husika kwa hatua za kisheria. "Hakuna upotevu wowote wa mapato unaotokea katika Bandari za Kigoma, tozo na makusanyo yoyote yapo kisheria na yamekuwa yakifanywa kwa kuzingatia sheria na taratibu za bandari," alisema Mabula.

Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Baraza ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, alizielekeza taasisi zinazohusika kuangalia uwezekano wa kuhuisha mifumo na taratibu zao, ili ikiwezekana tozo zote zikusanywe sehemu moja.

Alisema malalamiko ya Ahaji Mabie juu ya utolewaji wa Dola 25 hadi 30 hauendani na uwezo wa wadau wa eneo la Kibirizi na hauko katika mwongozo wowote wa tozo za taasisi za serikali zinazofanya kazi bandarini.

Katika mkutano huo, Alhaji Mabie, mfanyabiashara kutoka kampuni ya usafirishaji wa mizigo na abiria Aifola, alisema abiria wanaosafiri kwa kutumia meli za mizigo zilizoidhinishwa ili kupunguza changamoto za usafiri kuelekea nchini Congo, hutozwa kati ya Dola 25 hadi Dola 30 kama malipo ya tiketi, japo hawapewi tiketi za mashine ya EFD. "Bado wahusika wanatumia teknolojia ya zamani. Abiria hawakati tiketi katika mfumo maalumu, kinachofanyika wanaandikwa majina na mtu wa meli, wanatozwa Dola 25 au Dola 30 kisha anazichukua mtu anayekata tiketi na hakuna sehemu yoyote inayoonesha asilimia za tozo zinazoingia serikalini. Serikali iongeze usimamizi izuie mianya ya rushwa," alisema Mabie.

Alisema fedha nyingi zinapotea akitoa mfano wa fedha za udongo kiasi cha Dola tano zinazolipwa na wageni kutoka nchini Congo pindi waingiapo nchini ambazo hazina risiti wala maelezo yoyote, jambo linalofanya serikali ipoteze mapato mengi kupitia lango la uchumi na biashara la bandari.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa amemshika kaa wakati akipata maelezo kuhusu ufugaji wake kutoka kwa Kamishna wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Khamis Bakar Khamis, alipotembelea banda la chuo hicho, baada ya kufungua Maonesho ya Kilimo ya Nanenane katika viwanja vya Kizimbani, Wilaya ya Magharibi "A" Unguja, jana. **PICHA: IKULU**

# Mwabukusi atema cheche baada ya kula kiapo

**Na Waandishi Wetu**

RAIS mpya wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi, amesema TLS ina jukumu la kuhakikisha amri za mahakama zinaheshimiwa ili kutotengeneza kizazi kama GEN-Z kilichoko nchini Kenya.

Mwabukusi aliyasema hayo jana baada ya kuapishwa katika mkutano mkuu uliofanyika jana jijini Dodoma, siku moja baada ya kuchaguliwa kushika wadhifa huo.

Juzi, mawakili walipiga kura kuchagua Rais mpya na nafasi zingine ndani ya chama hicho na matokeo ya uchaguzi kutangazwa usiku. Hata hivyo, mmoja wa wagombea katika nafasi ya urais, Sweetbert Nkuba, ametangaza kwenda mahakamani kuyapinga kwa madai kuwa kulikuwa na ukiukwaji katika kutangaza matokeo.

Mwabukusi alisema kama amri ambazo zimekuwa zikitolewa na mahakama nchini zitaendelea kutoheshimiwa, basi kuna hatari ya taifa kujenga kizazi ambacho kitakuwa na vurugu na maandamano kama ilivyo Kenya.

"Tukiendelea kukaa kimya vitendo hivi vya watu kupuuza amri za mahakama, wananchi watakosa imani na chombo hiki na kujenga kizazi cha GEN -Z ya Tanzania kama ilivyo sasa kwa majirani zetu Kenya.

"TLS tunalo jukumu kubwa sana kuona amri za mahakama zinaheshimiwa kwani mahakama ni chombo kinacho stahili kuheshimiwa sana, vinginevyo watu wataanza kutembea na mapanga.

"Kwa hiyo ni wajibu wetu kama mawakili kuhahakikisha amri za mahakama zinaheshimiwa, kuna sehemu mahakama ilitoa amri mtu atolewe, lakini hakutolewa sasa hali hii siyo nzuri kabisa kwa taifa," alisema.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, Mwabukusi alisema TLS ina wajibu wa kuhakikisha sheria na kanuni zinazingatiwa ili uwe huru na haki.

"Ni kazi ya TLS ili kupata viongozi wenye sifa na uchaguzi kuwa huru na haki na kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza katika uchaguzi mara kwa mara nchini," alisema.

Kadhalika, alisema TLS inahitaji kuishirikisha serikali kutambua haki za wananchi wake hasa katika masuala ya umiliki wa ardhi.

"Lazima TLS tuishirikishe serikali kutambua pia, wananchi wanahaki kama inahitaji kuwahamisha eneo fulani, lazima ijue kuwa wao pia, wanayohaki yao ya kumiliki maeneo hayo yenye historia ya maisha yao," alisema.

**MAKUNDI YAVUNJWE**

Kuhusu uchaguzi wa TLS, Mwabugusi aliwaeleza wanachama kuwa kampeni zimekwisha na kutaka makundi kuvunjwa ili TLS kirudi kuwa moja.

"Uchaguzi umepita ndugu zangu. makundi yote yanapaswa kuvunjwa ili tuwe na TLS moja. Usiamini uko sahihi aliyekukataa anahaki kikatiba kwa hiyo tusitishe makundi yetu sote," aliagiza.

Aidha, alisema katika uongozi wake TLS kitaongozwa kwa sheria, kanuni na taratibu walizojiwekea na si kwa msimamo wa mtu mmoja.

**HOJA ZA NKUBA**

Baada ya matokeo ya uchaguzi huo kutangazwa, Nkuba alisema hakubaliani nayo na tayari amewaagiza wanasheria wake kwenda mahakamani kupinga.

Mgombea huyo alidai kuwa anaamini kwamba uchaguzi huo umechakachuliwa kwa sababu pamoja na kamati ya uchaguzi kufahamu idadi ya wapigakura, haikupeleka karatasi za kutosha za kupigia kura, hivyo kulazimika kwenda kuchapisha zingine wakati uchaguzi ukiendelea.

Sababu nyingine, Nkuba aliitaja kuwa ni makubaliano yao yalikuwa mawakala kutoingia na vifaa vya mawasiliano katika chumba cha kuhesabia kura.

"Lakini katika hali ya kushangaza na kustaajabisha matokeo ya uchaguzi yalianza kutumwa mitandaoni na watu kuanza kumpongeza mtu aliyesadikika kuwa ndiye ameshinda," alisema.

Mgombea huyo alidai kwamba hizo ni hujuma za kamati ya uchaguzi au kamati imeshirikiana na watu kuwapenyezea matokeo yasiyo rasmi na kuyatangaza nje na baadaye watu hao kufanya vurugu za kwenda kushinikiza kamati kutangaza matokeo wanayoyataka wao.

Nkuba alidai kuwa kamati ya uchaguzi au kwa kushirikiana na baadhi ya watu walishirikiana kuhujumu uchaguzi huo.

"Kwa hiyo ninaamini kamati imekosa weledi, msimamo na imehusika katika kuhujumu au kunajisi mchakato mzima wa uchaguzi kwa kutangaza matokeo ambayo hayaakisi uhalisia wa wapigakura na ubora wa kampeni na ubora wa mchakato ulivyokwenda. "Kwa taarifa hii, ninaomba kuujulisha umma kwamba, ninakwenda mahakamani kupinga mchakato huu wa uchaguzi na kupinga matokeo na kubatilisha ushindi uliotangazwa na kamati ya uchaguzi.

"Naamini mahakama itasimamia haki na kuufuta uchaguzi huu ili kuitisha uchaguzi mpya kwa ajili ya kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unafanyika kwa viwango na kwa kuzingatia weledi na usawa wa pande zote," alisema.

**UCHAGUZI ULIVYOKUWA**

Uchaguzi huo ulianza saa 12:30 asubuhi juzi katika Ukumbi wa Mikutano Jakaya Kikwete, Dodoma, ambako vituo kadhaa vya kupigia kura viliwekwa na mawakili walijitokeza kutimiza haki yao ya msingi, huku askari polisi wakisimamia usalama.

Mchakato huo ulitarajiwa kufungwa saa 6.00 mchana, lakini kabla ya muda huo, karatasi za kupigia kura zilikwisha na kusimama kusubiri nyingine na matokeo kutangazwa usiku.

Wagombea wengine waliokuwa wakiwania urais ndani ya chama hicho ni Emmanuel Muga, Paul Kaunda, Revocatus Kuuli na Kapteni Ibrahim Bendera.

**MAWAKILI WAPONGEZA**

Mmoja wa mawakili, Dawson Chacha, ambaye alishiriki mkutano huo, alisema walifurahishwa na matokeo hayo kwamba wamepata kiongozi waliokuwa wakimtaka muda mrefu.

Wakili Chacha alisema; "Kiongozi huyu ataongoza TLS kwa kipindi cha miaka mitatu tofauti na ilivyokuwa hapo awali, hivyo tunatarajia mambo makubwa hasa katika haki za mawakili, haki za wananchi, kwani kumekuwa na vitendo vya ukiukwaji wa haki kama vile ambavyo mmeona watu kutekwa na kupotea."

**Imeandaliwa na Paul Mabeja (Dodoma), Romana Mallya na Elizabert Zaya (Dar)**

# CCM yaita wanachama kuwania ubunge Bunge Afrika Mashariki

**Na Romana Mallya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewajulisha wanachama wake kwamba, yeyote mwenye nia na sifa ya kugombea ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki kujitokeza, ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi baada ya kifo cha Mbunge Dk. Shogo Sedoyeka.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, ilisema Katibu wa Bunge, amekijulisha CCM kuhusu ujazaji wa nafasi hiyo baada ya kifo cha Mheshimiwa Dk. Sedoyeka, kilichotokea Juni 13, mwaka huu.

Makalla alisema kwa mujibu wa Sheria, Bunge linatakiwa kufanya uchaguzi mdogo wa mbunge ili kujaza nafasi hiyo iliyowazi.

"Uchaguzi huo utafanyika wakati wa Mkutano wa 16 wa Bunge utakaoanza Agosti 27, mwaka huu," alisema,

Kutokana na hilo, Makalla alisema CCM kinawajulisha wanachama wake walio na nia na sifa za kugombea na kuchaguliwa kuwa mbunge wa Bunge hilo, mchakato wa kuchukua na kujaza fomu za maombi hayo ili kuteuliwa, utaanza Agosti 10, mwaka huu na kumalizika Agosti 15, mwaka huu.

"Fomu zitachukuliwa na kurejeshwa katika Ofisi za CCM kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 10 jioni. Mahali pa kuchukua fomu ni Makao Makuu ya CCM, Dodoma, Afisi Kuu ya CCM, Zanzibar na Ofisi Ndogo ya CCM, Dar es Salaam," alisema.

Makalla alisema CCM kinawahamasisha makada na wanachama wake kujitokeza kwa wingi katika mchakato huo ili kupata mwakilishi wa taifa katika bunge hilo kwa ustawi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.



Kondakta wa lori la mizigo lililokuwa limebeba lori jingine, akinyanyua nyaya za umeme kwa mikono bila kuvaa kinga yoyote ili lipite katika makutano ya Barabara ya Bagamoyo na Motisun, eneo la Mikocheni Viwandani, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wa maisha yake. **PICHA: JOHN BADI**

# Samia achoshwa matamko ya viongozi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan ameonesha kuchoshwa na matamko ya mara kwa mara ya viongozi katika ngazi mbalimbali serikalini, badala yake amewataka kuwa na ubunifu katika kutatua kero na kuwa na majawabu ya changamoto zinazowakabili wananchi.

Rais Samia alisema hayo jana wakati akizindua kampeni ya Tutunzane katika Uwanja wa Sokoine, Mvomero mkoani Morogoro iliyoasisiwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Judith Ngulil, ikiwa na kaulimbiu 'Mkulima Mtunze Mfugaji na Mfugaji Mtunze Mkulima Ili Kulinda Mazingira Yetu".

Kampeni hiyo inalenga pamoja na mambo mengine, kuwaelimisha wananchi hususani wafugaji kumiliki ardhi kwa lengo la kupanda malisho na kufuga mifugo michache kwa tija katika ardhi wanayomiliki na kutambua kila mmoja anamtegemea mwenzake kwa kile anachozalisha.

Samia alizitaka mamlaka za mikoa na wilaya kuhakikisha zinawasimamia vyema wenyeviti wa vijiji ili waache kupokea rushwa na kusaidia kuleta suluhu ya migogoro ya ardhi kwenye jamii na viongozi kutumia kampeni mbalimbali za suluhisho la amani badala ya kutoa matamko.

Rais alisema kilio kilichopo ni baadhi ya viongozi kushindwa kusimamia serikali za vijiji badala yake watu wakishaumizana huwa kichocheo rahisi kunyosha mkono kupokea badala ya kuleta suluhu. Aliwataka viongozi kuwasimamia wenyeviti wa vijiji ili walete suluhu za kweli za matatizo ya wananchi kwa kuzingatia sheria.

"Lakini kila mwananchi aheshimu uhuru wa mwenzake kwa kila shughuli anayoifanya ikiwamo kilimo na ufugaji kwani wote mnategemeana katika maisha ya kila siku. Mkulima amheshimu mfugaji na mfugaji amheshimu mkulima.

Wote mnazalisha na wote mnahitaji chakula kinachozalishwa," alisema.

Rais pia aliwataka wakuu wa wilaya na mikoa kuwachukulia hatua wale wote watakaoingilia uhuru wa watu kwa manufaa yao binafsi.

"Kama unataka kulisha mifugo, kalishe kwenye malisho siyo kwenye mashamba. Na nyie wakulima muache kukata mifugo ya wenzenu," alisisitiza.

Rais alionesha kuridhishwa na kampeni ya kimkakati ya Tutunzane wilayani Mvomero na kuahidi serikali kusimamia vyema na kuagiza uongozi wa mkoa, wilaya ya Mvomero, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo kuusimamia vyema mradi huo wa mfano kwa kutenga bajeti na kuwashirikisha wananchi kikamilifu.

Rais Samia alitumia mkutano huo kuwapatanisha wakulima na wafugaji kwa kuwataka wapeane mikono kama ishara ya kumaliza migogoro baina yao.

"Sasa wote mnakwenda kubadilika na kuingia kwenye mradi. Mkabadilike mlime mnaolima na mnaofuga mkafuge. Hakuna haja ya kugombana bali mtumie mradi huu kwani wote mnatupa uhai na mnatupa vitoweo na vyakula," alisema.

Aidha, alisema mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yakisababisha migogoro mingi ya wakulima na wafugaji hasa wakati wa ukame na kwamba kampeni hiyo inatarajiwa kuwa suluhisho kubwa katika suala hilo.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Nguli, alisema kampeni hiyo ya miaka mitano iliyoanza mwaka 2023, imeshawafikia zaidi ya wakulima na wafugaji 1,200 na kuwezesha uanzishaji wa zaidi ya mashamba ya malisho 40 sambamba yakiwamo ya ufuta.

Nguli alisema kampeni hiyo inakusudia kumaliza migogoro ya ardhi baina ya jamii hizo kwa kuhamasisha upandaji wa malisho ya mifugo, uchimbaji wa visima na malambo kwenye mashamba binafsi ya wafugaji, hamasa ya kilimo biashara na wananchi kuwa rafiki wa mazingira.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema katika kipindi cha miaka mitatu, wamejenga mnada wa kisasa uliogharimu Sh. milioni 500 eneo la Mkongeni wilayani Mvomero na kwa nchi nzima, imejengwa minada ya kisasa 51 iliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 17.5.

Pia alisema serikali imejenga majosho mawili ya mifugo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 36 wilayani Mvomero wakati nchi nzima majosho 742 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 17 yamejengwa.

"Tumesambaza dawa za kuogesha mifugo lita 230 za thamani ya Sh. milioni 10.5 kwa Mvomero wakati nchi nzima lita 180,000 zimesambazwa za thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 8.3, sambamba na madume bora ya mifugo 366 ya thamani zaidi ya Sh. milioni 100 nchi nzima," alisema.

Naye Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wanakusudia kutoa tani 50 kwa wakulima wa Mvomero na kuwataka waliojimilikisha maeneo bila kuyaendeleza kwenye skimu ya umwagiliaji Dakawa (UWAWAKUDA) watakokwa kupisha wananchi wa kawaida wanaotaka kulima.

Akiwa katika kiwanda cha Sukari cha Mtibwa na kuzindua bwawa la umwagiliaji na awamu ya tatu ya upanuzi wa mashamba na umwagiliaji, Rais Samia aliiagiza menejimenti ya kiwanda kuwashirikisha maofisa mazingira ngazi ya taifa katika ujenzi wa kwamba suala la mazingira litiliwe maanani.

Rais aliahidi kuwa serikali itaendelea kulinda makundi yote na inapotokea imeegemea upande mmoja wa wanyonge, upande mwingine usione vibaya kwa kuwa serikali inasimamia na kutetea maslahi ya makundi yote.

Alisema ikitokea sukari imepanda hadi Sh. 7,000 lazima serikali isimame na wananchi kwani ndio walaji na chakula ndio kila kitu. Alipongeza uongozi wa kiwanda cha Mtibwa kwa kutoa zaidi ya ajira 8,000 kwa vijana na ajira 9,000 kwa wakulima wa nje na kwamba upanuzi ukikamilika zitafikia ajira 11,000.

Aidha, Rais Samia alisema serikali katika kuthamini wawekezaji, imeondoa msamaha wa kodi Sh. bilioni 246 kwa viwanda vitano na kwa Mtibwa pekee, msamaha wa kodi ni Sh. bilioni 80.9 umetolewa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, Seif Ally Seif, alisema kiwanda hicho kinakabiliwa na changamoto ya umeme na kwamba kati ya pampu sita za maji katika bwawa hilo, ni mbili tu zinafanya kazi.

Alimwomba Rais Samia kuwaongezea uwezo wa umeme KVA 132 ambapo kwa sasa zipo 33 ambazo zinashindwa kuendesha pambu zote sita.

# Wahubiri ndani ya mabasi walivyogeuka kero

**Na Waandishi Wetu**

NENO la Mungu ni kila mahali. Ndivyo uhalisia katika nyakati za sasa kutokana na watu kuhubiriwa kila sehemu. Zamani ilikuwa imezoeleka makanisani au kwenye mikutano ya injili au makongamano lakini sasa ni kila mahali.

Ukienda kwnye vituo vya mabasi, wahubiri wamejaa. Kwenye mabasi ya abiria nddani ya miji kama Dar es Salaam, maarufu kama daladala, nako wako. Kwenye mabasi yanayotoka mkoa mmoja kwenda mwingine, nako wamejaa.

Watu hao wanafanya hivyo lakini jambo la kujiuliza inaruhusiwa? Wasio wa Imani hiyo, wanajisikiaje? Na je, wana vibali vya kufanya hivyo na mamlaka zinawatambua?

Iko marufuku ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) kwa watu wanaohubiri ndani ya mabasi au daladala, ikiambatana na faini ya Sh. 50,000 kwa wanaokiuka. Sheria ya LATRA haina meno?



Mkazi wa Dar es Salaam, akihubiri injili ya Yesu Kristo katika Kituo cha Daladala cha Shule, eneo la Tangi Bovu, Mbezi Beach Manispaa ya Kinondoni, juzi. **PICHA: JOHN BADI**

Uchunguzi wa Nipashe maeneo tofauti nchini umebaini huduma hizo zinaendelea kutolewa licha ya mwaka 2022 LATRA kusisitiza kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha kanuni za mamlaka hiyo.

Wakati baadhi ya abiria wakitaka kukomeshwa kwa huduma hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, akizungumza na gazeti hili jana, alisema wanaokutwa na kosa hilo faini huwa Sh. 50,000 au mahakamani.Suluo alisema nchi ni kubwa na idadi yao kulinganisha na daladala na mabasi ni ndogo, hivyo kuomba abiria wanapokutana na hali hiyo wawapigie simu kwa namba yao ambayo ni bure.

"Kuna wakati wenye mabasi wanasema si kweli, hivyo abiria awe na tiketi, tukishapata hizi taarifa huwa tunachukua hatua. Kosa huwa ni la dereva na kondakta wake.

"Utaratibu wetu kabla ya kumpa mtu adhabu, kwanza huwa tunatoa elimu, akipewa onyo inaingia kwenye kumbukumbu zetu kwamba, basi namba fulani lilipewa onyo, likijirudia mara ya pili huwa tunatoa adhabu kwa kumpiga kondakta faini ya Sh. 50,000 akiwa hana, inakwenda kwa mmiliki kama hajasajiliwa kwetu. Hii ni adhabu ya papo kwa hapo, asiporidhika tunampeleka mahakamani," alisema.

Hata hivyo, alitoa wito kwa abiria wanapoona vitu hivyo ni vyema kutoa taarifa kwa kumwajibisha mhusika kuwa anachofanya hakipo kisheria.

Mmoja wa abiria jijini Arusha, Amina Twaha, alisema katika huduma za usafiri hakuna mahubiri zaidi ya kuombwa fedha.

"Kuendelea kuwachwa maana yake unawaita madhehebu mengine nao waje, waganga wa kienyeji nao waje, wazee wa mila nao wafanye shughuli zao kwenye mabasi ya umma.

"Itakuwa ni fujo tu, kila mtu na imani yake aombe kimoyomoyo, siyo kufanya hivyo katika usafiri wa umma ambao unatoa huduma kwa watu wote bila kujali itikadi za dini tulizonazo," alisema. Shiisa Swai, mkazi wa Usa River, alisema mahubiri yana sehemu yake, ndiyo maana kuna misikiti na makanisa, wengine ni wapagani.

Mwananchi huyo alisisitiza kuwa katika mabasi kuna watu wa imani na madhehebu tofauti, hivyo si wote ambao wanapendezwa na mahubiri hayo.

Mwinjilisti Vivian James, alipoulizwa kuhusiana na katazo hilo la serikali, alisema; "Unajua wengine hawanaga muda wa kwenda kanisani au msikitini. Jamani huko ndiko wenzetu hao wanapopata hofu ya Mungu kupitia mahubiri hayo. Wako wanaoponya mioyo yao na si wote tunaotaka sadaka, tunafanya huduma."

Mkoani Kilimanjaro, baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Moshi, walisema uwapo wa watu wanaohubiri katika magari ni sawa na utapeli.

WAUZA DAWA NAO

Shane Samweli, mkazi wa Soweto, alionesha wasiwasi na watu hao akidai kwamba kama kweli ni wahubiri baada ya kuhubiri wasingekuwa wanaomba fedha.

"Hata kufanya biashara ya kuuza dawa za tiba mbadala kwenye mabasi nayo ipigwe marufuku. Serikali iwatoze faini madereva na makondakta wanaoruhusu watu hao kutoa huduma hiyo hizo kwa sababu hata kiwango cha sumu kwenye hizo dawa ni vigumu mtu kujua.

"Polisi na LATRA wabandike namba za maofisa wao ndani ya mabasi ambayo hayana ili abiria atakayewaona atoe taarifa kwa siri na basi likamatwe na kutoa adhabu ya kushindwa kuzingatia kanuni, kwa sababu wanaumiza hisia za mtu," alisema.

Jijini Tanga, wakazi wake wametaka serikali kuacha kigugumizi na kuchukuliwa hatua wahubiri wanaokiuka maagizo yanayotolewa.

Mariam colmani, mkazi wa Madina, alisema jambo hilo si sawa kutokana na wahubiri wengi huwakusanya watu eneo moja na kutoa neno la Mungu lakini wale ambao wanahubiri kwenye magari, hawajui kama wanavunja sheria.

Alisema kwa upande wake haoni ndani ya mabasi au daladala kama ni sehemu salama kwao kutoa mahubiri kwa sababu vyombo hivyo vya moto huwa kwenye mwendo.

Omari Fundi, mkazi wa Barabara ya 15, alitofautiana na wenzake na kusema endapo wahubiri hao wanapata fursa ya kuhubiri na hawavunji sheria, hakuna shida ya kueneza neno la Mungu.

Denis Chambi, mkazi wa Mabawa, alishukuru serikali kwa kuweka mazingira rafiki ya mtu kuabudu kwa imani yake.

**WAPIGWE MARUFUKU**

Jijini Dodoma baadhi ya wakazi wake, walisema kama serikali imepiga marufuku suala hilo na linaendelezwa sheria inapaswa kuchukua mkondo wake.

Nelson Matonya, alisema baadhi wamekuwa wakitoa mahubiri yanayokwanza wengine.

Neema John, mkazi wa Swaswa, alisema wahubiri hao wamekuwa wakihubiri pia, katika daladala na kuomba jambo hilo lifanyike katika maeneo maalum ya kuabudu au yaliyopewa vibali. Baadhi ya abiria hao kutoka katika kituo cha mabasi Kahama, akiwamo Sebastiani Mnakaya, walisema serikali inatakiwa kuwabana kutoa huduma hiyo ndani ya mabasi na badala yake wajenge makanisa sehemu ambazo hazina huduma hiyo ili kueneza neno la Mungu.

"Tunapata usumbufu tukiwa safarini, mtu husafiri kwa matatizo au mema ukiwa ndani ya basi mara usikie a mahubiri, mara wafanyabiashara wanatangaza biashara zao na wapo wanaolazimishwa kununua bidhaa au kutaka sadaka," alisema.

Rosemary William alisema changamoto hiyo iKo katika mabasi yaendayo Kahama-Mwanza, Kahama-Tabora, Bukoba-Mwanza, Kahama-Musoma na Kahama-Singida.

Alisema mwaka jana kaka yake wakati akielekea msibani Musoma, alitaka kupigana na mmoja wa wahubiri ndani ya basi kutokana na kulazimisha apewe fedha.

"Zamani mambo haya hayakuwapo, siku hizi huduma hizi zinaonekana kama biashara. Watu wanaojiita wachungaji wanaingia ndani ya mabasi kutoa mahubiri na kisha kutaka sadaka tu," alisema Nicodemas Charles.

Dereva wa basi moja linalofanya safari za Kahama-Tabora, Patrick Bundala, alisema wamekuwa wakiwaruhusu kama sehemu yao ya kujipatia kipato na kukanusha kuwa kwamba, hawana ubia wowote nao.

Bundala alisema watu hao hutoa neno la Mungu na hajawahi kusikia wakilazimisha abiria kutoa sadaka.

Mhudumu katika moja ya mabasi yanayofanya safari za Dodoma hadi Mwanza, Jessica Amon, alisema utaratibu huo wa wahubiri ndani ya mabasi wameukuta na kuendeleza kutokana na baadhi ya abiria huwa ni waumini.

Hata hivyo, alisema suala la utoaji wa sadaka huwa si la lazima kwa abiria na wanapomaliza hushuka na kuendelea na huduma kwingine.

# Biteko ataka mikataba uchimbaji wa makaa ya mawe inufaishe taifa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imesema haitakubali kuanza miradi mikubwa ya uchimbaji chuma na makaa ya mawe kabla ya kupata mikataba bora itakayonufaisha taifa.

Pia, imewatoa hofu wananchi mkoani hapa hususani Wilaya ya Ludewa kuwa madini ya makaa ya mawe na chuma yatachimbwa, lakini mikataba itakayoingiwa ni lazima iwe bora ikilenga kuwanufaisha.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, alitoa kauli hiyo juzi wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa uchimbaji wa madini ya chuma Maganga Matitu wilayani Ludewa, mkoani humo ulioingiwa kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) na Kampuni ya Fujian Hexingwang Industry Tanzania Co. Ltd.

Alisema serikali haiwezi kukubali wakati wowote kuona mgeni anafika nchini na kuchimba rasilimali halafu anaondoka huku akiwaacha wanashangaa na kuulizana kila mmoja kuwa imekuaje.

“Hatutakubali kuona uongozi wa mgodi au kiwanda kitakachojengwa viongozi wote wanatoka nje ya nchini, kwani hata mkataba ulioingiwa wa uchimbaji wa madini ya chuma tumekubaliana baadhi ya nafasi kushikwa na Watanzania na nyingine wageni,” alisema Biteko. Alisema hayo yote yatawezekana iwapo nchi itakuwa na amani ambayo itasaidia kuvutia wawekezaji.

Aliwataka wawekezaji waliopata nafasi ya kuwekeza nchini kuwa na uhakika na hawatopata hasara kwa sababu nchi ina mazingira mazuri ya kibiashara na mahali ambapo inaonekana kuna kasoro zinarekebishwa mara moja.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema mradi wa Maganga Matitu ulioko wilayani Ludewa una umuhimu mkubwa na kutegemewa katika kukuza uchumi wa nchi.

“Utekelezaji wa mradi huu, kwanza unatarajia kuwezesha ukuaji wa uchumi na kuchangia katika mnyororo wa thamani katika nchi yetu na ni matarajio kwamba, uchumi wa viwanda sasa unakwenda kukua,” alisema Kigahe.

Mkurugenzi Mtendaji wa NDC, Dk. Nicolous Shombe, alisema mradi huo wa uchimbaji wa madini ya chuma unaogharimu zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 77 ambazo ni mtaji kutoka kwa wawekezaji, ni wa kwanza hapa nchini ambao unakwenda kuchochea maendeleo ya viwanda.

“Tunatarajia mradi utachukua miaka mitatu kwa hiyo mwaka 2027 utaanza uzalishaji na wananchi wa pale ambao ni zaidi ya 300 wanakwenda kulipwa fidia ya Sh. bilioni 4.2 kabla ya mwezi Januari mwakani,” alisema Shombe.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema mkoa huo utaongoza kwa kuweka mazingira nafuu zaidi kwa kila atakayefika kwa ajili ya kuwekeza.

Naye Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema kitendo cha kutiwa saini mkataba huo kitafungua ulipaji wa wananchi kwa wananchi waliopisha mradi huo.

“Fidia za hawa ni chache tunaamini watalipwa mapema iwezekanavyo ili ujenzi uanze,” alisema.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kushoto), Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Anneth Komba (wa pili kushoto) na Mwandishi wa kitabu cha ‘A Tangled Web’, Eunice Urio (kulia), wakipiga makofi ikiwa ishara ya uzinduzi wa kitabu hicho, Dar es Salaam juzi, kinachoelimisha jamii juu ya athari za kusema uongo na matokeo yake, kupenda mali na fedha kwa kuzitafuta kwa njia isiyo halali na kufundisha namna ya kuwa na maadili na nidhamu ya maisha. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Serikali yabainisha fursa kwa waandishi wa vitabu

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imetenga fedha katika Bodi ya Maktaba ya Tanzania kwa ajili ya kununua vitabu vikiwamo ambavyo vitakuwa vimeshinda kwenye Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu ili kuhakikisha waandishi wanapoandika na kwenda kuchapisha wanapata faida.

Hayo yalibainishwa juzi usiku na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu cha A Tangled Web, iliyofanyika mkoani Dar es Salaam. Alisema kuna baadhi ya watu wanaogopa kuchapisha vitabu kwa kuhofia kupata hasara.

Alisema serikali bado inahimiza usomaji wa vitabu ndio maana imeanzisha tuzo ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu, kwamba wameweka mkakati pia wa kununua vitakavyothibitishwa kuwa ni vizuri na kuvipeleka kwenye shule. “Tuna kamati ambayo itakuwa inatushauri vitabu ambavyo tutakuwa tunavinunua kupitia Maktaba ya Taifa. Tungependa riwaya na hadithi za maisha kama za marais wastaafu tuone zinasomwa shuleni.

“Hii itachochea watu sio uandishi bunifu tu lakini kujua historia na kuchochea watu kuwa wajasiriamali kwa kuangalia maisha waliopitia, waandishi wanatunza historia, wanaweka kumbukumbu na utamaduni hivyo wanahitaji watunzwe na kuwapa kipaumbele,” alisema Prof. Mkenda.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Anneth Komba, alisema serikali imefanya mapitio makubwa ya mitaala ya elimu na katika mabadiliko hayo wamezindua ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya fasihi ya Kiswahili na ‘literature’ kuanzia kidato cha tatu.

Alisema masomo hayo yanatoa nafasi na fursa kwa waandishi kuandika vitabu vya kutosha ili ifike mahali watoto wasome riwaya zilizoandikwa na Watanzania, huku akimpongeza Eunice kwa uthubutu huo.

“Tuna uhitaji mkubwa wa vitabu vya hadithi za watoto na mashairi, kwa hiyo waandishi andikeni na mvilete taasisi ya elimu, tutavifanyia ithibati baada ya kujiridhisha vitatumika katika shule zetu,” alisema.

Mwandishi wa A Tangled Web, Eunice Urio, alisema kitabu hicho kinawalenga vijana na kina mafunzo mengi ikiwamo athari ya kusema uongo na matokeo yake, kupenda mali na fedha kwa kuzitafuta kwa njia ambayo sio halali, na kinafundisha namna ya mtu kuwa na maadili na nidhamu ya maisha.

Pia alisema wanakutana na changamoto nyingi ikiwamo ya rasilimali fedha, huku akitoa wito kwa serikali kuweka mazingira mnyororo wa thamani kwa waandishi wa vitabu ili kuwawezesha kufanya kazi yao iwe rahisi zaidi.

“Vitabu ndivyo vinaeleza utamaduni wetu, vinaweka kumbukumbu ya maisha yetu na zama tunazoishi, kwa hiyo watu wasipoandika ithibati mahali wataulizana zamani kulikuwa kunafanyika nini, ni muhimu watu waweke hizo kumbukumbu na pia ni njia ya kufundisha vizazi vijavyo na kuendeleza mila na desturi zetu,” alisema.

# Ujenzi vituo 77 polisi kukamilika

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imesema itakamilisha ujenzi wa vituo 77 vya polisi nchini vilivyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ili kusogeza karibu huduma kwa jamii hasa kwa wale wanaoifuata umbali mrefu.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, alisema hayo juzi katika ziara yake ya kikazi mkoani Mwanza baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Nyegezi, wilayani Nyamagana ambacho kilianzishwa kwa nguvu za wananchi hadi kufikia hatua ya linta.

Diwani wa Nyegezi, Edith Mudogo, alisema kutokana na kata hiyo kuwa na uhitaji mkubwa wa kituo cha polisi kwa ajili ya kupunguza vitendo vya uhalifu, walichangishana fedha ili kufikisha jengo hilo katika hatua ya boma.

Alisema kwa sasa ujenzi wake umesimama kwa kuwa ulitakiwa kukamilishwa na serikali ili kuanza kupata huduma, hivyo kumwomba Naibu Waziri Sillo serikali kutoa fedha ili kuharakisha ujenzi wa kituo hicho kukamilika mapema.

Naibu Waziri Sillo, pamoja na mambo mengine, alisema serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itahakikisha inakamilisha ujenzi wa vituo hivyo 77, kikiwamo cha Nyegezi.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2024/25, serikali itajenga vituo vingine vipya 12 kwenye kata mbalimbali pamoja na nyumba za askari polisi kwa kutumia fedha za mfuko wa tuzo na tozo.

Sillo alitembelea zahanati ya Jeshi la Polisi Mabatini inayotumiwa na jeshi hilo pamoja na wananchi ambayo kwa sasa inakabiliwa na ukosefu wa vifaa tiba na wodi ya wanaume na kuahidi kuhakikisha inaingizwa kwenye mipango ya maboresho kupitia wizara hiyo.

Mbunge wa Nyamagana, Stanslaus Mabula, alisema zahanati hiyo ina uhitaji mkubwa wa vifaa tiba na mashine mbalimbali za kufanyia vipimo vya kiafya, hivyo kuiomba serikali kupitia Wizara ya Afya na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kukifanyia marekebisho makubwa kwa kuwa kinatumika kama zahanati ya Kanda ya Ziwa.

“Zahanati hii inatumika kama Zahanati ya Kanda ya Ziwa inatumiwa sana na maofisa wa Jeshi la Polisi na wananchi, hivyo naomba muitizame kwa jicho la pili inahitaji maboresho na vifaa vya kufanyia huduma ukanda huu wote hakuna kituo kingine,” alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sarakasi za uchaguzi wa TLS zimekwisha, kilichobaki ni kazi

**HATIMAYE** Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kimefanya uchaguzi wa viongozi watakaokiongoza kwa miaka mitatu ijayo hadi mwaka 2027. Awali, viongozi waliokuwa wakichaguliwa kukiongoza chama hicho walikuwa wakidumu madarakani kwa mwaka mmoja tu na baada ya hapo walikuwa wanaweza kugombea kwa mara ya pili ya mwisho.

Katika nafasi ya urais wa TLS, kulikuwa na wagombea watano. Hata hivyo, mchuano ulikuwa mkali kwa mawakili Boniface Mwabukusi aliyeibuka kidedea kwenye uchaguzi huo na Sweetbert Nkuba aliyeshika nafasi ya pili. Mwabukusi amemshinda Nkubwa kwa zaidi ya kura 400 kwenye uchaguzi huo uliofanyika jijini Dodoma.

Joto la uchaguzi huo lilikuwa kali tangu mchakato wa kuanza wanachama kuchukua fomu kuwania nafasi hizo kuanzia ngazi ya kanda hadi taifa ambako wanachama walikuwa wakiwania nafasi za Rais, Makamu wa Rais na wajumbe wa bodi.

Moto zaidi ulikolezwa baada ya kamati ya rufani kumwengua Mwabukusi na hatimaye kufungua kesi Mahakama Kuu ya Tanzania masjala ya Dar es Salaam na hatimaye kushinda na kuwa miongoni mwa wagombea wa nafasi hiyo.

Hatua ya kuenguliwa kwake iliwagawa wanachama katika makundi mawili, wakiwamo wale waliokuwa wakitoa matamko bayana kwamba alikuwa ameonewa. Baadhi ya wanasheria na wadau wengine walikuwa wakidai kuwa kuenguliwa kwake kulitokana na sababu za kisiasa zaidi kutokana na kujipambanua kuwa yuko upande wa upinzani na amekuwa akiikosoa serikali kwa mambo mbalimbali.

Baada ya kurejeshwa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania urais kwa wakili huyo aliyejizolea umaarufu hivi karibuni hasa kutokana na sakata la uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam kwa kampuni ya DP World, kuliamsha ari ya mawakili mbalimbali na kutamka hadharani kwamba watakwenda Dodoma kumchagua.

Mchakato wa uchaguzi umekamilika na washindi wamepatikana na kama ilivyo ada katika demokrasia, panapokuwa na washindani lazima pawapo washindi na wanaoshindwa. Ndivyo ilivyotokea kwa TLS na jana Mwabukusi aliapishwa kuanza kutumikia nafasi hiyo huku pamoja na mambo mengine, akisisitiza kuwa uchaguzi umemalizika na watu wavunje makundi na kuwa kitu kimoja kwa maslahi ya chama.

Katika uchaguzi wowote ule, panapokuwa na pande tofauti, wakati wa mchakato ni lazima kuwapo na mikakati na mbinu za kutafuta ushindi na upande wenye mbinu na mikakati mizuri ndio unaoshinda na baada ya hapo lazima kuwapo na kukubali matokeo. Kupinga matokeo ni haki ya mtu lakini maslahi ya taasisi ni makubwa zaidi ya mtu au kikundi cha watu.

Ni kweli kama ni kitabu, sura ya uchaguzi imekwisha na sasa wana TLS wanapaswa kufungua sura mpya kwa ajili ya kukiendeleza chama chao kwa manufaa ya wanachama, Watanzania na taifa kwa ujumla. Hiyo inatokana na ukweli kwamba TLS ni nguzo muhimu kwa ustawi wa haki, sheria na utawala bora nchini. Kwa hiyo kuwapo kwa TLS imara ni ustawi wa demokrasia na utawala bora Tanzania.


Inawezekana kulikuwa na mawazo tofauti hata kudhani kuwa mmoja wa wagombea ni mwanaharakati, hivyo anaweza kusababisha nyufa ndani ya TLS na hata kuwapo kwa mivutano na watawala.

Pamoja na hayo, ni vyema ikafahamika kwamba TLS ni taasisi ambayo ina msaada mkubwa katika utungaji na utekelezaji wa sheria ambazo zinatungwa na bunge na kutekelezwa na dola pamoja na mahakama, hivyo inapaswa kutimiza jukumu lake badala ya kutumika na kundi fulani kwa maslahi yake.

Jambo la msingi na la kuzingatiwa ni kwamba mchakato wa uchaguzi ndani ya TLS umemalizika sasa ni nafasi ya waliochaguliwa kutekeleza majukumu yao. Kinachopaswa kufanyika ni kutekeleza majukumu kwa weledi na taaluma ili kuifanya Tanzania kuwa na demokrasia ya kweli, utawala bora na utawala wa sheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wanasiasa igeni jambo kutoka kwa Balozi Nchimbi

**TANGU** achaguliwe kuwa Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ameonyesha wazi msimamo kuwa si muumini wa kauli tata za wanasiasa zinazolenga kugawa Watanzania.

Yeye anaamini kuwa Watanzania wote ni wamoja bila kujali itikadi za vyama vyao, dini wala kabila na kwamba wanatakiwa kutukuza utanzania wao na kufanya kazi za kuleta maendeleo kwa pamoja.

Kutokana na msimamo huo, ni wazi kwamba wanasiasa wana cha kujifunza kutoka kwa mwanadiplomasia huyo kwa ajili ya kuendelea kudumisha umoja wa Watanzania.

Ninaamini kuwa kwa hekima, busara za Balozi hiyo, yeye ni hazina muhimu kwa chama chake. Hatua hiyo inakwenda sambamba na falsafa ya Mwenyekiti wa CCM Taifa Rais Samia Suluhu Hassan ya 4R.

Kiongozi huyo anasisitiza kuwa haoni aibu kuonyesha urafiki wake binafsi na wanasiasa wa vyama vya upinzani, lakini pia unakemea ubaguzi wa itikadi za vyama, kwa ustawi wa demokrasia.

Balozi Nchimbi anaamini kuwa msingi wa utanzania ni kuwapenda Watanzania wengine bila kuegemea kwenye ubaguzi wa kitikadi, rangi wala kabila, ambao uliasisiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Katika msimamo wake huo, hivi karibuni, aliwaonya viongozi wa CCM kutoa kauli za kibaguzi au kufanya vitendo vyenye taswira inayoweza kutafsiriwa kuwa wanashabikia ukandamizaji wa haki za wananchi.

Anasisitiza kuwa maneno na vitendo vya wana-CCM wakati wote lazima viakisi dhamana ambayo chama kimepewa na wananchi ya kuwatumikia, ikiwamo kusimamia haki, bila ubaguzi wala dhuluma ya aina yoyote.

Mwanadiplomasia huyo anasema, wanaCCM wanapaswa kulinda kwa wivu mkubwa ni taswira chanya ya CCM, hasa kuhusu dhamana ya kuongoza nchi na kuwatumikia wananchi kwa haki na usawa, kwa kupinga kauli na vitendo vya ubaguzi na dhuluma kwa Watanzania.

Binafsi ninaamini kuwa msimamo wake ni somo kwa wanasiasa wenye mihemko ambayo inasababisha watoe kauli zinazoashiria ubaguzi kwa sababu ya tofauti ya itikadi za vyama vya siasa.

Kimsingi, maendeleo hayana chama, ni jukumu la Watanzania wote kushiriki kwa pamoja katika shughuli mbalimbali, lakini bahati mbaya, wamekuwapo baadhi ya wanasiasa wenye kauli za kibaguzi.

Mfano, imekuwa ni kawaida kusikia baadhi ya wanasiasa wakisema, hadharani kuwa serikali haiwezi kuleta maendeleo sehemu ambayo wananchi wamechagua viongozi kutoka vyama vya upinzani.

Katika hili, ninaomba nieleweke kuwa sishabikii chama cha siasa, bali ninataka kuelezea kile ambacho kinaweza kusaidia kuwaunganisha Watanzania kama ambavyo mwanasiasa huyo anasisitiza.

Ingependeza kama vyama vingetumika kuhimiza maendeleo badala ya 'kuhubiri' utengano ambao mwisho wake ni kuwapo kwa chuki na uhasama, sababu ikiwa ni utofauti wa itikadi za kisiasa.

Kauli zinazokwenda kinyume na msimamo wa Balozi Dk. Nchimbi ambaye anaamini kuwa Watanzania wote ni wamoja bila kujali itikadi za kisiasa, kabila na aina nyingine yoyote, wanasiasa wasizipe nafasi.

Ninadhani wanaofuatilia mikutano yake watakuwa wamemsikia akisisitiza umuhimu wa Watanzania kuwa wamoja lakini pia wajumbe wa CCM kupitisha majina ya wagombea wanaokubalika kwa wananchi.

Hapa anagusa vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa vikitajwa kuwapo ndani ya chama hicho, wakati wa kura za maoni na kusababisha malalamiko kutoka kwa wanachama na wagombea wanaoachwa.

Katika hilo, msimamo wake huo unalenga kuchaguliwa kwa wagombea wenye nia ya kuwatumikia Watanzania, ili kuharakisha maendeleo ya nchi badala ya kuchagua wenye malengo binafsi.

**MAKALA**

**FIKRA MBADALA**

# Hongera Wakili Mwabukusi kuchaguliwa Rais TLS, kazi sasa kuhudumia wananchi



**Pascal Mayalla**

JUZI, kulifanyika uchaguzi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) , mmoja wa wagombea, alikuwa mtu 'asiyetakiwa' na zilifanyika juhudi mbalimbali kumkwamisha kugombea. Mahakama ndiyo ikaokoa jahazi kwa kumtendea haki. Huyu si mwingine bali ni Wakili Msomi Boniface Mwabukusi, ambaye amechaguliwa kwa kishindo. Kwa hiyo usiyemtaka kaja, itakuwaje?

Binafsi, nikiwa pia mwanasheria, wakili na mwanachama wa TLS, nimeufurahia ushindi huu, nikiamini ni Mungu ndiye amewezesha. Kuna jambo la kisheria Mungu anataka kulifanya kwa Watanzania, baada ya serikali yetu tukufu, kushindwa kulifanya tangu tulirejesha mfumo wa vyama vingi.

Ushindi wa Mwabukusi umepokewa na vifijo na nderemo ukumbi mzima, hivyo unatuma ujumbe mzito kwa waliokuwa hawamtaki kuwa sasa ndiye yeye, ndiye kaja. Nikiwa mwanachama wa TLS, si mara moja au mbili, nimeeleza kupitia maandiko yangu mbalimbali TLS inavyonyamazia madudu ya kisheria yanayofanywa na serikali, Bunge letu na Mahakama.

Kwa vile mgeni rasmi Mkutano Mkuu wa TLS alipangwa awe Rais Samia, mimi niliwaandikia waraka TLS, wamwambie nini Rais Samia. Hii ni sehemu ya waraka huo.

Hii maana yake ni Chama cha Mawakili Tanganyika kinaadhimisha miaka 70. Hiki ni moja ya vyama vikongwe kabisa vilivyoanzishwa hata kabla ya Tanganyika kupata uhuru. Kwenye majukumu ya TLS, naomba kujikita kwenye jukumu moja tu la kusaidia vyombo vya dola katika utungaji na utawala wa haki na utawala wa sheria.

Kabla sheria yoyote haijatungwa, TLS kama wadau wa sheria, inapitishwa kwao. TLS inatupa wanachama wote fursa ya kutoa maoni kisha kupeleka maoni yake ya kisheria, ndipo sheria inatungwa.

Ushauri wangu wa kwanza kwa Wakili Mwabukusi, kwa vile hakuna ubishi kumhusu yeye ni mwanaharakati, ombi la kwanza, asiigeuze TLS kuwa TLS ya kiharakati. TLS ni chama cha kitaaluma, hivyo mambo yake yaendeshwe kitaaluma na si kiharakati.

Kitu cha pili, aibadili TLS kutoka kuwa chama cha mawakili wasomi, kugeuka ni taasisi ya kuwahudumia wananchi, hivyo aishushe TLS kutoka huko juu iliko hadi chini kwa wananchi ikiwamo matumizi ya lugha yetu adhimu ya Kiswahili kwenye tovuti yake maana kwa sasa ni kimombo tu.

Tangu nimejiunga TLS kuwa mwanachama, nimekuwa nahudhuria vikao vya kukusanya maoni kuhusu ule mkataba wa IGA ya DPW na Bandari zetu, nikaipongeza TLS kwa maoni yake mazuri ya kisheria kwa mkataba ule. Lakini niliuliza swali kwa hili la Bandari, Pongezi TLS. Katiba yetu imenajisiwa. Bunge limetunga Sheria batili. Haki za Watanzania zimeporwa. Kwanini TLS wamenyamaza kimya? TLS ya Mwabukusi, hili si la kulinyamazia. Yakaja mabadiliko ya sheria ya uchaguzi. Kama kawaida, TLS ikatoa fursa kwa sisi wanachama wake kutoa maoni yetu. Siku ya siku serikali ikaitisha kikao kupokea maoni, TLS ikatoa maoni yake, serikali ikayapuuza na TLS wakanyamaza. TLS ya Mwabukusi, tukitoa maoni ya kisheria kwa serikali yetu, isipotusikiliza, tusinyamaze, tuibananishe kisheria.

Ubatili wa Katiba, Sheria na Kilio cha Haki.

Kwa muda mrefu, nimekuwa nikipigia kelele ubatili wa Katiba yetu, na ubatili wa sheria zetu uliopoka haki kuu ya msingi ya kuchagua na kuchaguliwa iliyotolowe na ibara ya 5 ya Katiba, inayompa kila Mtanzania haki na uhuru wa kuchagua viongozi anaowapenda kwa kuwapigia kura. Pia Ibara ya 21 inayompa kila Mtanzania haki na uhuru wa kushiri kwenye serikali, toka serikali ya mtaa hadi serikali kuu kwa haki ya kugombea uongozi, lakini haki hizo kuu mbili, zikaja kupokwa na ibara ya 39 na 63, zilizochomekewa ndani ya Katiba ambazo zinakwenda kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ya mwaka 1977.

wa mujibu wa katiba yetu hii yenye ubatili, haki ya kuchagua, yaani haki ya kupiga kura kumchagua kiongozi yeyote unayempenda imepokwa na kukasimiwa kwa vyama vya siasa, kuwa Mtanzania hayuko huru tena kumchagua kiongozi anayemtaka.

Analazimishwa amchague kiongozi aliyepitishwa na chama cha siasa. Pia kwenye kugombea uongozi, Mtanzania hana haki kwa mujibu wa Ibara ya 21, ili Mtanzania kugombea uongozi, analazimishwa ajiunge na chama cha siasa, hicho chama kimdhamini ndipo aruhusiwe kugombea!

Hili la ubatili wa Katiba ni jambo kubwa ambalo TLS ilibidi kishughulike nalo toka pale Mahakama Kuu iliutamka ubatili huo wa katiba na sheria hiyo ya TLS yetu ilinyamaza. TLS ya Mwabukusi hili si la kulinyamazia.

Naiomba sana TLS ya Mwabukusi iwe makini sana na ifanye kazi zake kwa weledi na kitaaluma zaidi. Ujio wa Rais Mwabukusi hii miaka 70 ya TLS ni fursa kwa TLS kutimiza wajibu wake kikamilifu kwa kuwawezesha Watanzania kupata haki zao zilizoporwa kipindi kirefu.

**Mungu Mbariki Mwabukusi,**
**Mungu Ibariki TLS**
**Mungu Ibariki Tanzania**
**Paskali**

# Shirika lakabidhi mradi wa maji wa mil. 425/-

**Na Beatrice Shayo**

SHIRIKA la WaterAid limekabidhi mradi wa uboreshaji wa huduma za miundombinu ya maji na usafi wa mazingira Hanang mkoani Manyara uliogharimu Sh. milioni 425 ambao unalenga kuwafikia wananchi 20,036.

Mkurugenzi Mkazi wa shirika hilo, Anna Mzinga, alisema hayo juzi wakati wa halfa ya makabidhiano ya mradi huo katika vijiji vya Bashang na Laghanga. Mradi huo ulikamilika ndani ya mwaka mmoja chini ya ufadhili wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Mzinga alisema Septemba, 2023 walizindua utekelezaji wa mradi huo mjini Katesh katika kikao cha wadau hatimaye kwa sasa umekamilika na wananchi kuanza kunufaika.

Pia alisema katika kikao hicho yapo mengi yaliwasilishwa na kujadiliwa kubwa lililobaki kwao kama taasisi lilikuwa lile la kuahidiwa ushirikiano wa dhati wa kitendaji, ushauri wa kiuongozi na ulinzi katika kutekeleza mradi huu.

"Tunakiri kupata ushirikiano mkubwa kutoka serikalini na wataalamu wote katika kutekeleza mradi huu na mpaka sasa umefanikiwa kukamilika kwa asilimia 100 kwa taasisi zote tatu zilizolengwa kwa mradi huu ikiwamo miundombinu ya vyoo bora, miundombinu ya usambazaji wa maji safi, miundombinu ya usafi binafsi na usafi wa kitaasisi na uelimishaji wa jamii ya watumiaji wa miundombinu," alisema.

Mzinga alisema WaterAid, ni taasisi isiyo ya kiserikali inayotekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na serikali ili kufikia watu katika maeneo mbalimbali ulimwenguni kwa huduma ya maji safi na salama, vyoo bora na mazingira salama ya usafi na usafi binafsi.

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki, Leah Kaguara, alisema WaterAid inafanya kazi kwa kushirikiana na serikali kuhakikisha kuwa kila mtu anafikiwa na huduma za maji salama, usafi wa mazingira na usafi.

Alisema WaterAid ilizindua mkakati wake mpya wa kimataifa mwaka 2022 na programu za nchi za Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na Tanzania zilitengeneza na kuzindua mikakati yao mwaka 2023.

"Lengo letu la kwanza katika mkakati huu kusaidia kupatikana kwa huduma za maji, usafi wa mazingira na usafi (WASH) ziwe endelevu inayojumuisha na salama, huduma katika eneo la Wilaya ya Hanang kwa ajili ya mabadiliko mapana huku lengo la pili likilenga kuweka kipaumbele cha WASH katika sekta ya afya ili kuboresha afya ya umma," alisema.

Alisema wataendelea kufanya kazi mjini Hanang ili kuunga mkono mipango ya serikali ambayo inalenga kuhakikisha kila mtu katika wilaya hiyo anakuwa na huduma endelevu zinazojumuisha WASH.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ya Hanang, Athuman Likeyekeye, alishukuru kwa mradi huo na kueleza kuwa miundombinu yote iliyopangwa kutekelezwa imekamilika vizuri na ipo tayari kwa matumizi.

Alisema mradi huo utawanufaisha wananchi wa Kata ya Laghanga, Wareta na maeneo ya jirani wakiwamo wanafunzi na wagonjwa.

# Wakulima, wafugaji, wavuvi kunufaika na uwapo wa vyuo

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAKULIMA, wafugaji na wavuvi wa mikoa ya Kanda ya Mashariki ambayo ni Morogoro, Tanga, Dar es Salaam na Pwani, wameelezwa kuwa wana kila sababu ya kufanya vizuri kutokana na kubarikiwa kuwa na taasisi kubwa za sekta hizo katika mikoa yao.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batlida Buriani, alisema hayo juzi wakati akifungua Maonesho ya Wakulima, Wafugaji na Wavuvi, maarufu kama Nanenane Kanda ya Mashariki yanayofanyika katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, mkoani hapa.

Alisema katika sekta ya kilimo, mkoa wa Morogoro kuna Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na taasisi mbalimbali za utafiti wa kilimo na kwamba endapo wakulima watavitumia kikamilifu wataongeza uzalishaji na tija, hivyo kulingizia taifa mapato.

"Wenzetu wa SUA hapa Morogoro wamekuwa wakitoa mchango mkubwa katika sekta ya kilimo, hivyo wakulima wakija katika maonesho haya watafaidika na kila elimu wanayotaka kuhusu kilimo, hivyo hakuna sababu ya sisi Mikoa ya Kanda ya Mashariki kushindwa kufanya vizuri," alisema.

Kuhusu mifugo, Balozi Dk. Buriani alisema kwenye mkoa wa Tanga kuna Taasisi ya Kitaifa ya Mifugo (TARIRI) ambayo wafugaji wa Kanda ya Mashariki wana uwezo wa kuitumia kwa ajili ya kuboresha mifugo yao ikiwemo kunenepesha na kufuga kisasa.

Akizungumzia uvuvi, alisema kwa mkoa wa Dar es Salaam ipo Taaisisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) ambayo imekuwa ikitoa mchango mkubwa kuimarisha sekta hiyo, hivyo hakuna sababu ya kushindwa kufanya vizuri.

Mkuu huyo wa mkoa alisema asilimia 65 ya Watanzania kwa sasa wako kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ambazo wanachangia pato la Taifa asilimia 28 kutokana na bidhaa wanazozalisha na asilimia 24 kuuzwa nje ya nchi.

Kuhusu maonesho hayo, alisema kila mwaka yamekuwa yakiimarika kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotembelea kwa ajili ya kujifunza teknolojia mbalimbali za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Alisema mwaka 2023, watu 75,000 walitembelea maonesho hayo na mwaka huu wanategemea yatatembelewa na watu zaidi ya 80,000 huku idadi ya washiriki ikiongezeka kutoka 589 mwaka 2023 na kufikia 596 mwaka 2024.

# Naibu Waziri apata mapokezi makubwa

**Na Mwandishi Wetu**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, amepata mapokezi makubwa jimboni kwake, Kwela, Sumbawanga mkoani Rukwa baada ya kuwasili kwa mara ya kwanza tangu ateuliwe katika nafasi hiyo, na kuwashukuru wananchi kwa mapokezi hayo.

Aidha, amewahakikishia wananchi kuwa atafanya kazi kwa weledi na uaminifu wa hali ya juu huku akimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa heshima kubwa aliyowapa wananchi wa Kwela na Rukwa kwa kumteua kuwa Naibu Waziri wa ofisi yake.

Sangu alisema hayo kwa nyakati tofauti juzi wakati akizungumza na watumishi na wananchi katika kata za Kanda na Kaengesa kwenye mikutano ya hadhara iliyofanyika kwenye vijiji vitano jimboni humo.

Alisema Rais Samia amewaheshimisha wananchi wa mkoa wa Rukwa kwa kumteua ili kumsaidia kuwahudumia Watanzania katika masuala ya utumishi na utawala bora.

"Naomba niwaahidi katika najukumu yangu haya mapya nitakuwa mnyenyekevu, mchapakazi, mweledi na mwaminifu katika kumsaidia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene.

"Nawashukuru pia wananchi wa Kwela kwa kuniamini na kunituma bungeni ili nikawasemee changamoto zinazowakabili. Hii ilisababisha Rais Samia kuniona na kuniteua kushika wadhifa huu," alisema.

Katika hatua nyingine, Sangu alimshukuru Rais kwa kutekeleza miradi mingi ya maendeleo katika Jimbo la Kwela ikiwamo ujenzi wa zahanati, barabara, maji na umeme.

"Mambo mazuri zaidi yanakuja. Rais Samia amesema anataka kuiona Kwela yenye nuru kiuchumi," alisema.

Alisema Rais anawapenda wananchi wake husussan wa mkoa wa Rukwa ndiyo maana ameongeza bei ya mahindi hadi Sh. 700 kwa kilo moja ili kuhakikisha wananchi wa Kwela wananufaika kiuchumi kupitia kilimo cha zao hilo.

Hata hivyo, Sangu aliowaonya wananchi wasithubutu kuuza mazao yote la sivyo kufikia Januari, mwakani, watakumbwa na baa la njaa.




Wananchi waliofika kwenye banda la Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, wakipata msaada wa sheria kutoka kwa wanasheria mbalimbali katika Maonesho ya Kilimo Nanenane yanayoendelea mkoani Morogoro jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wananchi wanavyonufaika na msaada wa kisheria ziara ya Samia Morogoro

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan yuko katika ziara ya kikazi mkoani Morogoro kwa ajili ya kukagua shughuli za maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

Kiongozi huyo wa nchi, katika ziara yake hiyo ya siku sita, mpaka sasa ameshatembelea wilaya za Gairo, Kilosa, Mvomero na leo anatarajiwa kuwasili wilayani Kilombero.

Aidha, timu ya wanasheria wa kampeni ya msaada ya kisheria ya Samia, maarufu kama Mama Samia Legal Aid, imo katika ziara hiyo kwa ajili ya kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ufuatiliaji Haki wa Wizara ya Katiba na Sheria, Beatrice Mpembo, anasema wameambatana na Rais Samia ili kusikiliza na kutatua changamoto za wananchi wanaohitaji msaada wa kisheria.

"Tutakuwa na Rais muda wote wa ziara hapa Morogoro na tuko na Waziri wetu, Pindi Chana, na wasaidizi wa kisheria ngazi ya wilaya na mkoa. Kila anapofika Rais, kama kuna mtu ana changamoto ya kisheria tunaichukua na kuifanyia kazi.

"Kupitia ziara hii, tumeshatoa msaada wa kisheria kwa wananchi mbalimbali na hata jamii ya Wamasai tumekutana nao kwenye maeneo mbalimbali na tumewapa elimu ya sheria kuhusu migogoro yao ya mara kwa mara ya ardhi," anasema.

Mpembo anasema wakati wanasheria wengine wakiwa kwenye ziara hiyo, Rais Samia ametuma wanasheria wengine kupitia Kampeni ya Mama Samia Legail Aid kutoa huduma za msaada wa kisheria kwenye maonyesho ya Nanenane mkoani humo.

Anasema timu ya wanasheria hao iliwasili mkoani Morogoro juzi na inaendelea na kazi ya kuwahudumia wananchi mbalimbali ambao wanamatatizo ya kisheria kwa kuwapa msaada wa kisheria.

Tangu wanasheria hao wawasili kwenye viwanja vya Nanenane mkoani Morogoro, wananchi wengi wamekuwa wakifika kwenye banda la Mama Samia Legal Aid katika maonesho hayo na wamekuwa wakipewa msaada wa kisheria.

Mmoja wa wananchi aliyepata huduma ya msaada wa kisheria, Jerome Kiangi, anampongeza Rais Samia kwa uamuzi wake wa kuwasaidia wananchi wasio na uwezo wa kutatua matatizo yao ya kisheria.

"Kwa kweli nampongeza Rais Samia kwa upendo wake kwa Watanzania amegundua kwamba wengi wetu tunahitaji msaada wa kisheria. Nimekuja hapa nimesikilizwa na wanasheria na wamesema tatizo langu la mgogoro wa nyumba litapatiwa ufumbuzi. Namshukuru sana," anasema.

Mwananchi mwingine, John Lubeja, anapongeza hatua ya Rais Samia kutuma wanasheria kwenye maonesho hayo kwa kuwa wamekuwa mkombozi kwa wananchi ambao hawana uwezo wa kupata huduma za kisheria.

"Kupata wakili ni gharama sana. Kwa hiyo huduma kama hizi zinaposogezwa karibu na wananchi kama hapa kwenye maonesho, tena bure, ni jambo la faraja sana na la kupongeza mno," anasema Lubeja.

Hivi karibuni, Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Ester Msambazi, alisema kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Legal, inatarajiwa kuanza kutikisa mikoa 19 kuanzia mwezi huu ili kuhakikisha wananchi ambao hawana uwezo wa kifedha wanapata msaada wa kisheria.

Alisema kwenye mwaka wa fedha ulioisha walifanikiwa kuwafikia wananchi 500,000 na kwamba wameshapanga ratiba ya namna ya kuhakikisha wanaifikia mikoa yote iliyobaki.

"Tumeshapanga kila mwezi angalau tumalize mkoa mmoja kwa hiyo wananchi wawe na amani kwamba sisi tutawafikia kupitia kampeni hii mikoa yote ambayo hatujapita tutahakikisha tunapita mmoja baada ya mwingine," alisema.

Msambazi alisema kwenye kampeni hiyo wanashirikiana na wadau mbalimbali kama Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA) na Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania Bar Association.

Alisema mbali na wadau hao, mpango huo unafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi kupitia Dawati la Jinsia.

"Kwenye kampeni hii tumepata ushirikiano mkubwa sana wa mahakama, Jeshi la Magereza nao wamekuwa wakiratibu vizuri namna ya sisi kuwafikia wafungwa na mahabusu na kuwapa msaada wa kisheria na wadau wengine tunaomba tuendelee kusaidiana kufanikisha jukumu hili zito la kusaidia wananchi," alisema.

Alisema pia wamekuwa wakifanyakazi kwa karibu na wasaidizi wa kisheria paralegals na aliwaomba kuendelea kushirikiana na serikali ili iwe rahisi kuwasogezea huduma za msaada wa sheria kwani wengi hawana uwezo wa kumudu kuweka mawakili kwenye mashauri yao.

Aliwataka wasaidizi wa sheria ambao wako kwenye mikoa mbalimbali nchini wajitoe kwa nguvu zao zote kuwasaidia wananchi kwa kuwaandalia nyaraka za kuwasilisha mahakamani na kuwashauri namna ya kupata haki zao.

"Pia wahakikishe wanawapatia usuluhishi wa migogoro yao kwasababu kuna aina ya migogoro ambayo mnaweza kukaa nao mkazungumza na mkafikia mwafaka hata bila ya kufikishana mahakamani," alisema.

Alisema huduma hiyo ni endelevu na wasaidizi wa kisheria watakuwa wanapita kwenye mikoa mbalimbali hata ile ambayo wamepita kuwapa elimu wananchi kuhusu masuala ya kisheria.

Mama Samia Legal Aid Campain ilizinduliwa Aprili, mwaka jana, kwa kuanzia mkoa wa Dodoma na mpaka sasa tayari mikoa saba imefikiwa. Mingine ni Manyara, Singida, Simiyu, Shinyanga na Njombe na Ruvuma.

# MAISHA

AGOSTI 4, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Yajue matumizi ya uma, vijiko vyako

Ukurasa 15




# HARUSI YAKO

Ukurasa 12

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | K | W | E | T | U |
| ■ | W | ■ | ■ | W | ■ |
| B | E | I | ■ | A | ■ |
| ■ | N | ■ | A | N | A |
| ■ | Y | ■ | ■ | G | ■ |
| T | E | N | G | A | ■ |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
LIA, TOA, TAMBO, SHAKA, KOKOTO, SHINDA


## AMSHA AKILI



## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## CHEKA



**Alichokifanya daktari**

MTOTO Juma na rafiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukumuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Wivu wa mke unavyochangia mume kufa mapema

KARIBU tena msomaji wangu kwenye safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Hapa tunachambua mambo mbalimbali yanayojiri kwenye familia zetu kila uchao. Si hadithi bali ni kweli na yanatokea.

Wiki kadhaa zilizopita, nimejadili sana kuhusu kinachochangia mwanamume kufa mapema. Bado nazidi kuchimbua eneo hilo nikitoa mifano zaidi na nini kifanyike. Wivu ni moja ya vyanzo vilivyojificha pasipo wengi kufahamu.

Kufa kupo kwa aina mbili, kimwili na kiroho. Na kufa kwa binadamu kunaanzia rohoni ndipo kunajitokeza kimwili. Ulimwengu wa roho (usioonekana) ndio unaotawala ulimwengu wa kimwili (unaoonekana kwa macho ya nyama).

Kinababa wengi ambao walitakiwa kuwa mhimili wa familia, wamekuwa wa kawaida kutokana na kupumbazwa na wake zao waliowanyang'anya ukuu wao. Wako wanaume wanaonekana barabarani lakini "walishauawa" na wake zao kitambo na wao hawajui. Wake zao wanawalaghai kwa wivu kumbe wanaharakisha kufa kwao mapema pasipo kujua. Hebu sikia mfano huu.

Yuko mama mmoja rafiki yangu ambaye ni mfanyabiashara au kwa maneno mengine mjasiriamali. Mume wake ni wale wanaokaa vijiweni kwa kazi za kubangaiza, japokuwa anazo nguvu za kufanya kazi kubwa zaidi.

Mwanamke ni mchakarikaji na wamebarikiwa kuwa na watoto watatu, wawili wako ngazi ya sekondari na mdogo shule ya msingi. Mama amejiingiza kwenye vikundi vya kukopeshana (vikoba) ambako hupata ada za shule na mahitaji mengine.

Mumewe mara nyingi yuko nyumbani na hata akionekana kwenye biashara ya mkewe ni mara chache. Kipindi cha mwaka jana, biashara ilikuwa ngumu, hata kulipa marejesho ya mikopo kukawa kugumu.

Kibaya zaidi hivi karibuni eneo anakofanyia biashara likachukuliwa na mamlaka ya jiji na wafanyabiashara wote wakaamrishwa kuondoka. Kimbembe kikawa kutafuta eneo lingine na hela ya kodi ikawa ngumu.

Aliponisimulia yote hayo nikamuuliza: "Mume wako ana mchango gani katika kukusaidia utokane na sintofahamu hiyo?" Akajibu mumewe hachangii chochote kwa kuwa mahitaji yote ni yeye anatoa.

Nilipodadisi zaidi nikaambiwa kwamba mama huyu ana wivu sana na mume wake. Hapendi atoke sana nyumbani na hata akitoka lazima ajue yuko wapi na anafanya nini.

Sasa maisha yamebadilika, biashara imeanguka hana msaada. Kwa nini hakumshirikisha mume katika yale ayafanyayo usimamizi ukawa imara kwa mambo makubwa ya kuingiza kipato?

Shida hapa ni mama huyu kujifanya anaweza na pia kuchukua nafasi ya mume wake, jambo ambalo hata Mungu ameshaweka wazi kwenye neno lake. Mithali 31:3 "Usiwape wanawake nguvu zako; Wala moyo wako usiwape wale waharibio wafalme."

Kingine wako wanawake wanaowaonea wivu waume zao na kwenda kuwafunga kwa waganga wa kienyeji eti watulie nyumbani wasitafute mahusiano nje ya ndoa. Tabia hii imeharibu wanaume wengi wamekuwa mazuzu hawafanyi chochote.

Hawa wamefungwa ufahamu na hatua zao, hivyo hawawezi kupiga hatua yoyote na kujikuta wanakaa tu nyumbani. Mwanamke anatamba amemuweza kumbe ndio ameharibu hata uchumi wa familia.

Wanaume wengi wanakufa mapema kwa sababu mwanamke hakusimama kwenye nafasi yake. Yeye badala ya kuwa mlinzi wa mume, amechukua nafasi yake kujiona anaweza yote. Neno la Mungu linasema, Yeremia 31:22 "...Kwa maana BWANA ameumba jambo jipya duniani; mwanamke atamlinda mwanaume".

Pia Mungu kuna mahali anawaonya wanaume pale anaposema, waishi na wake zenu kwa akili na wanawake waishi na waume zao kwa hekima. Kama mwanamke ni mlinzi wa mwanaume halafu mwanamke huyo huyo anamfunga asipige hatua unategemea nini hapo?

Kama mwanamke hatasimama kwenye nafasi yake kama msaidizi na mume akasimama nafasi yake ya kichwa/nguzo ya familia, nyumba itayumba tu. Hiyo ni kwa sababu maagizo ya Mungu yamekiukwa!

Ifahamike pia utajiri wa mwanaume upo kwa mwanamke. Pale mwanamke anapomtia moyo mume wake katika majukumu yake ya kuingiza mapato ya familia, ndivyo mafanikio makubwa yanavyoonekana.

Ndiyo maana ya ule msemo kwamba ukiona mafanikio ya mwanamume ujue yupo mwanamke pembeni mwake anayemsaidia, kumtia moyo na hata kumlinda.

Pia mwanamke akitoa madhaifu ya mume wake kwa watu wengine anamuua mapema. Huyo atadharauliwa na wenzake na kujisikia mnyonge. Wengi wanakufa mapema kwa mifadhaiko (stress) hasa pale msaidizi(mke) wake anapokaa pembeni.

**Tuishie hapa hadi wiki ijayo. Je, una maoni, Kisa? Tuma ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Hawa wanaokopesha pesa mfuko wa shati hawaonekani?

PESA za moto. Huko mtaani ndilo jina wanalolijua zaidi Watanzania, lakini sina hakika kama serikali inawajua na inawaona.

Kuna watu wanaojiita wafanyabiashara wanaokopesha pesa za riba kubwa mitaani lakini hawana ofisi na hawana kibali cha kubadilishia fedha. Hawa ni kausha damu walioboreshwa zaidi.

Ni miungu watu fulani hivi. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) hawa wanaokopesha pesa za riba hamuwajui?

Usilogwe ukope pesa kwao kwa kuacha kadi ya gari au kuweka dhamana ya mali. Siku unataka kurejesha pesa zao ili umalize mkataba naye huwa hapatikani.

Anachotaka akikufuata ni mambo mawili, kwamba umeshindwa kutimiza matakwa ya makubaliano na mali yako ndio imepotea ili kufidia pesa yake aliyokupa.

Wamekuwa matajiri, hawalipi kodi ya serikali. Hizo ndizo pesa za moto wanavyoziita. Hivi watu hawa wanalipa wapi kodi ya serikali? Wanajulikana idadi yao? Je, wanafanya utakatishaji au ni uhujumu uchumi?

Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, inasemaje kuhusu hao wanaokopesha pesa za riba mitaani?

Wengi wanatamani serikali ifanye kitu kukomesha biashara hiyo kwa kuwa inaumiza na inaacha Watanzania wengi masikini.

Moto walioanza nao Jeshi la Polisi nchini wiki iliyopita, usiishie Arusha wala usiwahusu tu wanaofanya biashara ya kunadili fedha za kigeni, uguse hata hawa wanaokopesha pesa kwa kificho.

Jeshi la Polisi wiki iliyopita lilimnasa mfanyabiashara mmoja mkazi wa Sanawari mkoani Arusha, Samweli Mbise (42), akiwa anafanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni bila ya kuwa na kibali.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani humo, Justine Masejo, mtuhumiwa huyo alikamatwa katika operesheni maalum ya ukamataji wa watu wanaofanya biashara hiyo ya kubadili fedha za kigeni bila ya kuwa na kibali.

Polisi inasema mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa na fedha mbalimbali za kigeni pamoja na fedha za Tanzania. Kati ya fedha hizo, zimo Dola za Marekani 5,952, Euro 835 na Dola za Canada 1,845. Pia alikuwa na Paundi 45, Swiss Franc 20, Dola za Australia 50 na Quatar Riyals 05.

Nyingine ni Paundi za Misri 25, Shilingi za Kenya 38,400 na Sh. Za Tanzania 52,552,000ambazo jumla yake ni Sh. 75,8096,49.

Masejo amenukuliwa akisema: "Tunaendelea na upelelezi wa shauri hili, pindi upelelezi utakapokamilika jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

> **"Wamekuwa matajiri, hawalipi kodi ya serikali. Hizo ndizo pesa za moto wanavyoziita. Hivi watu hawa wanalipa wapi kodi ya serikali? Wanajulikana idadi yao? Je, wanafanya utakatishaji au ni uhujumu uchumi?**

"Sambamba na hilo, tunatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili mkoa wetu uendelee kuwa shwari."

Swali langu, ni je ni hao peke yako wanaofanya makosa ya kufanya biashara ya pesa bila kibali?

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akisisitiza kila wakati kwamba tujifunze kutanguliza maslahi ya taifa mbele.

Wako wanaoliibia taifa, wanafanya uhujumu uchumi wakitanguliza matumbo yao yasiyoshiba. Hawa watu wanapesa na wanazipata isivyo halali.Kibaya zaidi ni matajiri kuliko. Hakuna tajiri mtiifu kwa masikini, huu nao ni wizi.

**•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI









Ilikuwa siku ya furaha kwa Bwana na Bibi Cassian baada ya kufunga ndoa takatifu hivi karibuni na kufuatia sherehe ya aina yake iliyofanyika jijini Mwanza. PICHA: McGaraB.

MITINDO

Na Moshi Lusonzo

# HATA KIKOI KINATOSHA


KIKOI ni moja ya kitambaa cha kitamaduni kinapendwa kuvaliwa na watu wa rika na jinsia zote.

Vazi hili ambalo chimbuko lake ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki, lilianza kutumika miaka mingi na kila siku mwonekano wake hubadilika kutokana na mahitaji ya watu.

Aina hii ya nguo licha ya kuvaliwa kitamaduni, lakini wabunifu wamefanya kuwa na mabadiliko makubwa baada ya kubuni mitindo mbalimbali ya mavazi kwa kutumia kitambaa cha kikoi.

Kikoi kimetengenezwa kwa pamba na kuwekwa nakshi ya michoro, kisha hufumwa badala ya kuwekwa rangi.

Nje ya matumizi yaliyokusudiwa kama vazi rasmi, hutumika kubebea mtoto mgongoni, taulo au kitambaa cha kufungia kichwani.





UREMBO

Na Mary Geofrey

# NDIZI MBIVU NA UREMBO

MBALI na kuliwa kama tunda ndizi mbivu zina manufaa mengine hasa katika urembo wa ngozi.

Ndizi zina virutubisho muhimu vinavyoboresha ngozi.

Hakikisha unanawa uso wako mara tatu kwa siku. Unapofanya hivyo unaondoa uchafu.

**Huzuia chunusi**

Hakikisha unanawa uso kwa sabuni ambayo inaendana na ngozi yako.

Ikiwa ngozi yako ni ya mafuta, hakikisha unatumia sabuni ambayo itakuacha ukiwa mkavu na kama ngozi yako ina ukavu, jioshe na sabuni itakayokufanya uwe na unyevu.

**Kulainisha ngozi**

Changanya asali na ndizi moja iliyopondwa na upake kwenye uso na shingo.

Nawa uso kwa maji baada ya muda wa nusu saa. Fanya hivi angalau mara moja kwa wiki.

**Kung'arisha uso**

Ndizi huwa na Vitamin C ambayo husaidia kuiweka ngozi kuonekana iking'aa.

Kwenye ndizi iliyopondwa, ongeza vijiko viwili vidogo vya juisi ya limau na upake kwa uso na shingo.

Osha kwa maji ya fufutende baada ya dakika 20. Ni vizuri kupaka mchanganyiko huu wakati unapoenda kulala.

**Kuzuia mikunjo**

Ponda parachichi na ndizi pamoja na paka kwa uso na uoshe baada ya muda.

Mchanganyiko huo hulainisha ngozi ya uso na kuwa laini lakini hupunguza ukubwa wa matundu ya ngozi ya uso wako.


**Husaidia kuzuia chunusi**


Hakikisha unanawa uso kwa sabuni ambayo inaendana na ngozi yako. Ikiwa ngozi yako ni ya mafuta, hakikisha unatumia sabuni ambayo itakuacha ukiwa mkavu na kama ngozi yako ina ukavu, jioshe na sabuni itakayokufanya uwe na unyevu.


**Kulainisha ngozi**

Changanya asali na ndizi moja iliyopondwa na upake kwenye uso na shingo. Nawa uso kwa maji ya fufutende baada ya muda wa nusu saa. Fanya hivi angalau mara moja kwa wiki.









MAPISHI

Na Mary Geofrey

# FURAHIA MTORI

MTORI ni moja kati ya chakula maarufu kinachotumika wakati wa asubuhi kwa watu wazima na watoto.

Chakula hiki kimejizolea umaarufu mwingi sehemu mbalimbali nchini, huku kikisindikizwa na vitafunwa mbalimbali kama chapati na maandazi.

Kwa watoto wadogo, wagonjwa na wazazi waliotoka kujifungua chakula hiki kimekuwa sehemu ya mlo wao wa siku unaowapatia nguvu na ladha ya kipekee.

Kuna aina mbalimbali za mapishi ya chakula hiki. Mapishi ya mtori kwa kutumia kipekecho (kifaa cha asili kinacho tumika kusaga chakula), blenda au kusaga kawaida na mwiko.

Leo tutajifunza aina hizo tatu rahisi ambazo unaweza kupika nyumbani na ukaachana na habari ya kununua mgahawani au hotelini.

Mara baada ya nyama na ndizi kuiva anza kwa kuweka ndizi kwenye



bakuli safi au sufuria kisha uziponde ndizi kwa kipekecho taratibu na kuondoa mabonge yote.

Baada ya hapo anza kusaga kwa kupekecha taratibu huku unaongeza supu ya nyama taratibu mpaka ndizi zako zilainike kabisa.

Rudia hatua hiyo mpaka uridhishwe na ulaini wa mtori wako kisha rudisha jikoni ongeza supu iliyobaki, mafuta ya kupikia chumvi, kitunguu, karoti, hoho na uache uive kwa dakika tano na mtori wako utakuwa tayari.

Kusaga na blenda

Aina hii ya mapishi inafaa sana kwa watu wenye haraka, unachotakiwa kufanya ni kuweka ndizi zako zilizoiva kwenye blenda, ongeza supu na usage mpaka zilainike.

Hakikisha ndizi zako zimepoa ndipo usage pia uweke kidogo kidogo ikiwa una ndizi nyingi.

Baada ya hapo mimina mchanganyiko wako kwenye sufuria ongeza supu iliyobaki, mafuta ya kupikia kiasi, chumvi, kitunguu, karoti hoho na uache uive kwa dakika tano na mtori wako utakuwa tayari kwa kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# TAMBUA MAGONJWA HATARI KWENYE NYUMBA

KAMA ilivyo kwa viumbe hai kuathiriwa na mazingira wanayoishi, ndivyo ilivyo pia kwa viumbe visivyo hai ikiwamo nyumba.

Binadamu hukumbwa na magonjwa mbalimbali na ndivyo viumbe visivyo hao kama nyumba ndivyo vinavyopata maradhi pia. Nyumba hukumbwa na magonjwa mbalimbali ambayo kama hayatapatiwa tiba mapema, kuna uwezekano wa nyumba kubomoka au kuharibika wakati wowote na kuwa hasara kwa mmiliki.

Ili kuepuka majengo yasiathirike, ni vyema ubunifu wake ufanyike katika hali ya ubora wa hali ya juu katika sehemu husika linapojengwa jengo.

Msanifu majengo, Deodatus Kwivilo, anasema hata ujenge nyumba nzuri na kubwa kiasi gani, kama haijabuniwa na kujengwa kwa kuzingatia mazingira ya eneo husika, lazima iwe hatarini kuathirika.

Kwivilo anasema kabla ya kuanza kujenga nyumba ni lazima ufanye uchunguzi katika eneo husika kubainia endapo kuna magonjwa yanayoweza kuathiri nyumba yako na kufanya ubunifu wa kukabiliana nayo.

Mtaalamu huyo anasema endapo nyumba hiyo itajengwa pasipokufanyiwa ubunifu mzuri huenda ikaathiriwa na magonjwa hayo.

Anasema miongoni mwa magonjwa yanayoathiri nyumba endapo haijafanyiwa ubunifu mzuri ni kutitia.

Kwamba mara nyingi hutitia kutokana na aina tofauti za udongo, kiwanja au kimo cha msawazo wa msingi kuwa tofauti pamoja na ubunifu hafifu wa udongo kulingana na uzito wa jengo husika.

Ugonjwa mwingine anasema ni nyumba kupitisha maji, na kwamba maeneo mengi ya Tanzania yamezungukwa na vyanzo vya maji ambayo yanahitaji usanifu na ubunifu wa hali ya juu wakati wa ujenzi wa nyumba ili kuepuka athari baadaye.


"Maeneo mengi ya Pwani majengo yake mengi yameathiriwa na tatizo hili na hata limekuwa kero kwa wakazi na watumiaji wa majengo hayo. Baadhi ya majengo yanapitisha maji kwa njia ya sakafu na kuta mithili ya chujio au chemchemu na mara nyingi utagundua kwa kuona ardhi yake inatoa maji wakati wote wa majira ya mwaka.

"Na majengo mengi ya maeneo haya yanaoza na kutitia kwa haraka na hata mashimo ya vyoo vyake huinuka kwenda juu ambalo ni hatari kwa afya za wakazi. Katika hali hii kuta na sakafu huoza kwa haraka kutokana na maji yaliyopo chini ya ardhi kuwa na kemikali mbalimbali zilizopo kwenye maji hayo. Kwa hiyo katika mazingira haya lazima yatumike malighafi sahihi za kuzuia maji hasa wakati wa ujenzi," anasema.

Lingine, anasema ni kuoza kwa nyumba na kwamba hali hiyo hutokana na unyevunyevu na kemikali mbalimbali kupitia maji kukaa kwa muda mrefu kwenye kuta na kuathiri ubora wa kuta hizo.

"Na hii husababisha kumea kwa mimea ambayo kusababisha ukungu wa kijani kwenye kuta ambao huzalisha fangasi mbalimbali wanaokula kuta," anabainisha.





## Yajue matumizi ya uma, vijiko vyako

Na Restuta James

FAMILIA nyingi hasa za mijini hazikosi uma, visu na vijiko vya aina mbalimbali, japokuwa matumizi yake hayako bayana sana.

Mtaalamu wa mpangilio wa nyumba, Brigitte Didas, anasema watu wengi wana vyombo vizuri ambavyo havitumiki.

Anatoa mfano kwamba familia nyingi zinatumia visu vya kulia chakula kwa ajili ya kupaka siagi kwenye mkate.

"Ni nadra kukuta chakula kimeandaliwa kwa vyombo kuwekwa kwenye mpangilio unaofaa. Mfano, uma, kisu na kijiko ni vitu vya kawaida vinavyopaswa kuwekwa mezani ili mtu achague anachoona kinafaa," anasema.


Briggite anasema vijiko ni kwa ajili ya supu na vyakula vya 'stater' wakati uma na kisu ni kwa chakula (main dish) kama wali au ugali pamoja na 'dessert' ambavyo ni ice-cream au cake.

"Kila chakula kina aina yake ya kijiko, uma au kisu. Ni vitu vya kawaida ambavyo sio vibaya mara moja moja kufanyika kwenye mlo...kwa wanaojua hayo ni maisha yao na ni jambo zuri," anasema.

Anashauri kwamba matumizi ya vitu hivyo yanapaswa kufundishwa kwa watoto tangu wakiwa wadogo.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...SAFARI YA FUKARA HAINA MAPUMZIKO...

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani kupeleka meli, ndege vita kuilinda Israel

**WASHINGTON,** MAREKANI

HALI ya wasiwasi inazidi kutanda Mashariki ya Kati, huku Marekani ikiimarisha jeshi lake kwa kupeleka meli na ndege za kivita kuilinda Israel.

Marekani inachukua hatua hiyo baada ya kuwapo kwa tishio kutoka Iran ambayo imeahidi kulipiza kisasi kwa Israel kufuatia mauaji ya aliyekuwa kiongozi wa Hamas, Islail Haniyeh yaliyofanyika mji mkuu wa Tehran. Taarifa ilisema uwepo wake wa kijeshi kwenye kanda ya Mashariki ya Kati kwa kupeleka meli na ndege za ziada za kivita ni kwa ajili ya kuwalinda wafanyakazi wa Marekani na Israel.

Wizara ya Ulinzi ya Marekani, ilitoa tangazo hilo baada ya Iran na washirika wake wa kikanda kuapa kulipiza kisasi kufuatia mauaji hayo na kamanda wa Hezbollah aliyeuawa katika mji wa Beirut nchini Lebanon. Mapema wiki hii, Israel ilimuua kamanda wa Hezbollah, Fuad Shukr, hatua ambayo Israel ilisema ilikuwa ni jibu la shambulizi la roketi lililofanywa na kundi hilo wiki iliyopita kwenye milima ya Golan. Saa chache baadaye, kiongozi wa Hamas, Ismail Haniyeh aliuawa katika mji mkuu wa Iran, shambulio ambalo Israel bado imejizuia kulizungumzia hadi sasa.

Hata hivyo, Ofisa wa ngazi ya juu wa idara ya usalama wa Israel, alionya kwamba nchi hiyo haitojizuia ikiwa Iran itaishambulia.

Kulingana na ofisa huyo Israel haitosita kujibu mashambulizi hayo ya kulipiza kisasi kufuatia mauaji ya kiongozi wa Hamas, Haniyeh ambaye aliyezikwa jana mjini Doha, nchini Qatar.

Tzachi Hanegbi, mshauri wa usalama wa Israel alilinganisha mvutano wa sasa na ule uliojitokeza Aprili, wakati Iran iliilenga Israel kwa mashambulizi makubwa ya droni zipatazo 330 na makombora ya masafa marefu.

Hanegbi alisisitiza kwamba kwa sasa hali ni tofauti na kuwa Israel ilijizuia mara moja na haitoweza kufanya hivyo mara mbili huku akisisitiza kuwa yeyote atakayeishambulia Israel atalipia gharama kubwa.

Hofu imekuwa ikiongezeka kuhusu hatari ya kutanuka kwa mzozo huo na kulitumbukiza eneo zima la Mashariki ya Kati katika vita vya kikanda. Kiongozi Mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, aliapa kulipiza kisasi kufuatia mauaji ya Hanniyeh katika ardhi yake. Wiki hii Marekani iliihakikishia Israel kwamba itaisaidia kulinda usalama wake na kukabiliana na vitisho vyote kutoka kwa Iran.

**DW.**



Raia wakibeba mwili wa mtu aliyeuawa katika shambulizi lililofanyika ufukweni mwa eneo la Lido nchini Somalia jana. **PICHA: REUTERS**

# Watu 32 wauawa Somalia

**MOGADISHU,** SOMALIA

WATU 32 wameuawa na wengine 63 wamejeruhiwa katika shambulio lililotokea jana katika eneo la ufukwe wa mji mkuu wa Somalia, Mogadishu.

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi nchini humo ilisema shambulio hilo lilitokea katika ufukwe maarufu wa Lido ambao hufurika mamia ya wakazi wa Mogadishu kwa ajili ya mapumziko ya mwisho wa juma.

Msemaji wa polisi nchini humo, HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/al-shabaab-yashambulia-kambi-za-jeshi-somalia-na-kuwaua-watu-25/a-69310703" Abdifatah Aden alisema mshambuliaji mmoja alijilipua mwenyewe, watatu waliuawa katika majibizano ya risasi na mmoja alikamatwa.

Eneo la Lido limekuwa likilengwa na mashambulizi ya mara kwa mara, ikiwamo tukio la wanamgambo Al-Shabaab kuizingira hoteli moja ya kifahari mwaka 2023. Kwenye mkasa huo watu sita waliuawa na wengine 10 kujeruhiwa.

**DW**

# Kamala Harris achaguliwa mgombea wa Democrat

**CHICAGO,** MAREKANI

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, amechaguliwa kuwa mgombea wa Chama cha Democrat baada ya kupata kura nyingi.

Baada ya kuchaguliwa, Harris aliwaambia wafuasi wa chama hicho kuwa anaichukulia kwa heshima kubwa nafasi hiyo ambayo anaweza kuwa mteule.

Kongamano la Kitaifa la Chama cha Democratic ambalo litamthibitisha Harris, litakalofanyika Chicago mwezi huu.

Harris ni mwanamke wa kwanza Mwafrika na wa kwanza kutoka Asia Kusini, kupeperusha bendera ya chama cha kisiasa nchini Marekani kuelekea Ikulu ya White House.

Ikiwa atamshinda Donald Trump, mgombea wa chama cha Republican katika uchaguzi wa Novemba, atakuwa rais wa kwanza mwanamke Marekani.

Alichaguliwa bila kupingwa katika uchaguzi huo baada ya Rais Joe Biden, kujiondoa mwezi uliopita na kumuunga mkono kuwania nafasi hiyo.

Juzi washindani wake kadhaa walifuata mkondo huo na kumpongeza na kumfanya Harris kuwa mgombea rasmi baada ya kupata uungwaji mkono kutoka kwa wajumbe 2,350, idadi inayohitajika kuteuliwa.

**BBC**

# Jeshi kutumika kuvunja maandamano Nigeria

**ABUJA,** NIGERIA

JESHI la Polisi nchini Nigeria, linafikiria kuomba msaada kutoka vikosi vya jeshi baada ya maandamano ya kupinga gharama ya maisha na serikali kugeuka kuwa ghasia katika baadhi ya miji.

Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali, Kayode Egbetokun, alisema kama maandamano hayo yataendelea kuwa ghasia kuna uwezekano wa kuomba msaada kutoka jeshini.

Waandamanaji watatu waliuawa kaskazini mwa jimbo la Kadunasiku ya Alhamisi, waandishi wa habari wa Reuters walisema.

Amnesty International ilisema juzi kuwa waandamanaji 13 kwa jumla waliuawa katika majimbo matatu ya kaskazini, lakini mamlaka haijatoa maoni yoyote juu ya vifo vyovyote. Baadhi ya miji mikubwa, ikiwa Abuja na Kano kaskazini ilionekana kuwa shwari siku moja baada ya polisi na waandamanaji kupigana. Hata hivyo, maandamano zaidi yanatarajiwa kufanyika huku watu wakiwa na hasira kuhusu mageuzi ya kiuchumi ya Rais Bola Tinubu ambayo yameongeza ugumu wa maisha kwa raia wa kawaida nchini humo.

IGP Egbetokun, alisema polisi walikuwa wamehamasishwa kikamilifu na tayari kujibu haraka vitisho vyovyote vya kuvunja utulivu wa umma.

"Kwa kuzingatia hali ya sasa, Jeshi la Polisi la Nigeria limeweka vitengo vyote kwenye tahadhari," alisema Egbetokun.

Aliendelea "Polisi wameandaliwa kujibu ipasavyo hali inayoendelea na watapata usaidizi kutoka kwa vyombo vingine vya usalama, ikiwa ni pamoja na jeshi ikiwa hitaji litatokea."

**DW**

## MAKALA

# UZALENDO HAUTAKUWA NA MAANA KAMA HAYA HAYATAONEKANA WAZI



Na Magabilo Masambu

NIMESIKIA baadhi ya watu wakipendekeza kuwa katika shule zetu za msingi na sekondari pengine na vyuo, kuwapo na somo linaitwa uzalendo. Ni mawazo mazuri kwa sababu hii inaonyesha uwapo wa pengo la uzalendo miongoni mwetu.

Nawaunga mkono katika kutafuta njia za kufanya ili Watanzania katika ngazi zote kuwa wazalendo katika nchi kama si wazalendo. Pamoja na kuwaunga mkono, sina hakika kama wamefanya utafiti wa kutosha kujua sababu za kuwapo kwa ombwe la Watanzania kutokuwa wazalendo na wanaposema Watanzania si wazalendo wanatazama nini.

Katika jambo hili la uzalendo, iko mitazamo mingi kila mtu akijaribu kutoa tafsiri ya uzalendo kwake ni ipi. Wako wanaoona uzalendo ni kuwa machawa wa kusifu kila jambo linalofanya na kiongozi wa serikali au wa chama chake. Wako wanaoona uzalendo haupo kwa sababu baadhi ya viongozi na wananchi wanasadikika kutumia vibaya mali za nchi kwa maslahi binafsi. Pia wako wanaodhani kwamba ukiwa kiongozi ukawa na mali wewe si mzalendo, hata kama mali hizo unazipata kihalali ili mradi una mali.

Wako wengine wanaodhani kwamba uzalendo ni kuishi maisha ya umaskini na hasa unapokuwa kiongozi na dhana hii imekuwapo mioyoni mwa Watanzania wengi kudhani kwamba ukiwa kiongozi unatakiwa kuwa maskini ili uonekane mzalendo. Wako wanaoonekana si wazalendo tu kwa sababu wanawakosoa baadhi ya viongozi katika serikali kwa utekelezaji wao wa baadhi ya mambo katika nafasi zao. Najaribu kujiuliza na nataka hata wale wanaotaka shule zifundishe somo la uzalendo wajiulize je, kwa pamoja tunafahamu tafsiri ya uzalendo kwa nchi ni nini?

Pamoja na tafsiri nyingi tulizo nazo kuhusu uzalendo, nadhani kwa mtazamo wangu, mambo yafuatayo yanaweza kusaidia katika kujenga uzalendo wa wananchi na viongozi katika nchi yoyote ikiwa yataonekana kwa macho na kama hayataonekana waziwazi basi kazi ya kufundisha somo linaloitwa uzalendo itakuwa sawa na kuchota maji ziwani au baharini kwa kutumia tenga kwa sababu uzalendo ni vitendo.

Moja ni juu ya haki. Tunafahamu kwamba katika nchi zinazoongozwa kwa mujibu wa sheria, namaanisha zenye Katiba na mahakama zisizoongozwa kwa maelekezo ya mfalme, haki isipopatikana mtaani basi itapatikana mahakamani. Viongozi wenye dhamana wakiongoza kwa haki bila uonevu na kila mtu akaona kwa macho kwamba haki inatendeka iwe kwa viongozi wenye dhamana au mahakama basi watu wakishajenga imani hiyo watakuwa wazalendo.

Pili, uadilifu wa viongozi. Nimesema uzalendo unahusianishwa na umaskini kwamba ukiwa kiongozi hutakiwi kuwa na mali. Kuna ukweli kwa maana moja kama uliingia madarakani ukiwa maskini mara ghafla mwenzetu umekuwa tajiri, basi suala la kutokuwa mwadilifu linaweza kuwapo. Lakini kama ulikuwa tajiri kabla ya uongozi na utajiri huo ni wa haki si wa dhuluma na wizi, wale unaowaongoza wanaweza kuwa wazalendo kutetea nchi au kukutetea wewe, lakini wanajua kabisa hukuwa na kitu umetajirikia kwenye uongozi halafu unataka watu wawe wazalendo huku wewe ni mwizi, usitegemee viongozi wenzako au wananchi watakuwa wazalendo. Nao watatafuta namna ya kutajirika na kama wewe.

Katika nchi mkishakuwa na sheria zinazokandamiza watu katika nyanja mbalimbali, iwe kwenye biashara labda sheria za kodi, elimu, uongozi na maeneo mengine mengi, mtawafanya watu watafute njia nyingine za kurahisisha maisha kwa namna ambayo inaweza kuleta athari katika nchi. Kama ni kodi watatafuta njia za kukwepa kulipa.

Tatu, wananchi kuwa sehemu ya maendeleo ya nchi. Hii ina maana kwamba kama wananchi ndio wanaochagua viongozi na ndio wanaolipa kodi ili nchi ijiendeshe, wanatakiwa kuwa na nguvu za kisheria za kuwaajibisha viongozi wao badala ya viongozi kuwa mabwana na wananchi wawe watwana. Wananchi wasigeuke kuwa watumwa au watumishi katika nchi yao bali viongozi ndio wanatakiwa kuwa watumishi wa wananchi.

Mambo ya kusema unanijua mimi nani, wakati unayemuuliza ndiye aliyekuweka hapo, inapoteza dhana ya wananchi kuwawajibisha viongozi wasiofaa na uzalendo wa wananchi unaanza kupotea hapo na mwisho wa siku wanaona kumbe wao si sehemu ya maendeleo ya nchi. Kila kitu kinachofanyika ndani ya nchi, lazima ionekane kwamba kimefanywa na wananchi na hiyo itawafanya wajione kwamba wao ndiyo wanaofanya si mwingine yeyote itawapa moyo wa kuendelea kujitolea kujenga nchi yao kwa moyo.

Jambo la nne, thamani ya waliopita. Nchi ni kama famlia na ukikuta familia fulani ni tajiri hawakuzaliwa na utajiri huo, kuna watu katika familia hiyo walifanya kazi usiku na mchana na walijinyima na wakati mwingine walihatarisha maisha yao ili familia isimame kiuchumi. Lakini mara nyingi watoto wanaozaliwa katika familia hizo huwa wanadhani vitu vilikuwapo tu toka dunia iumbwe, na kwa sababu hawajui mali zilipatikanaje baadhi wanazifuja sana kulewa, kufanyia mambo ya ovyo na wakati mwingine kutowakumbuka hata wazee wao waliozitengeneza na kutozitumia ovyo ili hao watoto wanufanike.

Katika nchi yoyote kuna watu wema kabisa ambao walikuwa waaminifu kwa kiasi ambacho hakiwezi kuelezeka, hivyo hawakuwa matajiri wakati huo lakini pengine kwa sababu hawako kwenye nafasi, wamekuwa watazamaji wakiwa wamejikunyata pembeni mwa viota vya moto. Nani anawajua, wanatambuliwa kwa namna gani juu ya mchango walioutoa kwa nchi husika ili utambuzi huo uwafanye walioko sasa wafanye kazi kwa uadilifu wakiamini siku watakapoishiwa nguvu watakuwa na vijana watakaowatambua?

Mfano katika nchi yetu tuna utaratibu wa kuwalipa mafao ya uzeeni watumishi walio katika mfumo rasmi, je, ni kweli ndiyo pekee wanajenga nchi hii? Wale wasiyokuwa katika mfumo rasmi wanaoshiriki kwa jasho na machozi mafao yao ya uzeeni ni yapi? Mchango wao wa kushiriki katika ujenzi wa nchi yetu unatambuliwaje ili kuwafanya vijana wasio katika mfumo rasmi wajenge nchi kwa moyo?

Itoshe kusema yako mambo mengi ambayo yakionekana kwa macho yatawafanya wananchi wote kubadilika na kujifunza taratibu namna ya kujenga uzalendo. Sina hakika kama ndilo somo lenyewe hilo linalotakiwa kufundishwa. Katika makala ijayo, nitaeleza nini kinatakiwa kufanyika badala ya kufikiria kila kitu kipelekwe kwenye mtaala.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Wakongo nao pia waliiga sana nyimbo za Wabongo enzi hizo*



Na Adam Fungamwango

NI ukweli usiopingika kuwa wanamuziki wa Tanzania waliziiga sana nyimbo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo miaka ya nyuma, kuanzia miaka ya 1960 mpaka 2000.

Nianze kutoka mifano ya baadhi ya nyimbo zilizoigwa ambao ni maarufu ni ule ulioitwa 'Napenda Nipate Lau Nafasi.' Huu ni wimbo wa Kilwa Jazz Band ulivyochukuliwa kutoka kwenye wimbo wa 'Mokolo Nakokufa' wa African Fiesta, ukiimbwa na Tabu Ley Rochereau mwanzoni mwa miaka ya 1960.

Kilwa Jazz hao hao, wakaiga wimbo mwingine wa TP OK Jazz, chini ya Franco Luambi Luanzo Makiadi uliotwao 'Course au Pouvoir'.

Dar Jazz nao wakaiga wimbo wa TP OK Jazz ya Franco uitwao 'Quatre Boutons', wao wakauita 'Mtoto Aacha kupiga Mayowe' na Ndala Kasheba, akiwa na Orchestra Safari Sound mwanzoni mwa miaka ya 1980, alirekodi wimbo ulioitwa "Uliomba Tucheze' ambao aliuiga kutoka pia TP OK Jazz, utunzi wake Ntesa Dalientst uliitwao 'Bina Ngai na Respect', yaani cheza na mimi kwa nidhamu.

Hizo ni baadhi ya nyimbo nyingi ambazo wanamuziki kutoka Tanzania haijalishi ni Watanzania au Wakongomani waliziiga kutoka Congo DR, wakati huo ikiitwa Zaire.

Hata hivyo si wengi wanaofahamu kuwa hata wanamuziki wa Congo, wameziiga sana nyimbo za wanamuziki wa Tanzania. Tukianza na wimbo wa 'Dada Asha' uliopigwa na Tabora Jazz Band, uliigwa mara nyingi zaidi na bendi nyingi za Zaire wakati huo kwa mujibu wa Tabu Ley alipofanya ziara mwaka 1987. Kwanza alishangaa sana kusikia wimbo huo ni wa Tanzania, akasema kule kwao Zaire, bendi nyingi zinaupiga wimbo huo na ziko zilizourekodi pia.

Katikati ya miaka ya 1980, Soukous Stars ikiwa na kina Ngouma Lokito, Dally Kimoko, Lokassa ya Mbongo, Shimita Lukombo Nzambi na wengine, walirekodi wimbo huo, kwenye albamu yao ya 'Nairobi Night'.

Ni kundi hilo hilo na kwenye albamu hiyo hiyo, pia zilirekodiwa nyimbo za 'Western Jazz' uitwao 'Vigelegele Ndiyo Furaha' na Roza ambazo ulipigwa na bendi hiyo mwanzoni mwa miaka ya 1970.

Kundi hilo ambalo pia lilikuwa na mwamuziki kama Saladin Ferreira ambaye wengi wanadhani ni Mkongomani, lakini huyu ni raia wa Afrika ya Kati, ambapo alizaliwa jijini Bangui, ndiyo maana kwenye baadhi ya nyimbo zao ambazo amepiga solo, au rhythm, kuna vipande ambavyo wanamtaja 'Saladin, Saladin, mwana Bagui'. Wengine ni Yondo Sister, Lucien Bokilo na Balou Canta.

Kundi hilo lilirekodi nyimbo hizo bila ridhaa ya bendi au watunzi wa nyimbo hizo.Walipofanya ziara miaka ya 1990, walipoulizwa walisema nyimbo hizo walizinunua nchini Kenya.

Hawakufahamu kuwa ni nyimbo zilizopigwa na bendi za Kitanzania, badala yake wakadhani kuwa zilikuwa za bendi za Kenya na hata waliowapa ruhusa ya kutumia nyimbo hizo, yaani waliokuwa wamiliki hati miliki za nyimbo hizo walikuwa nchini humo.

Hawakupata tabu sana kwa nyimbo za Western Jazz kwa sababu bendi yenyewe ilishakufa na wanamuziki wengi kusambaratika, wengi wakiwa hawapigi tena muziki, lakini kwa wimbo wa 'Dada Asha' kazi walikuwa nayo, kwani mtunzi Shem Karenga akiwa bado yu hai, aliwakalia kooni.

Kwa ujanja wa Wakongomani, walichofanya ni kumjumuisha kwenye kundi lao la Soukous Stars na kuanza kuzunguka naye nchi nzima, hii ikazima joto la kuendelea kudai haki zake kwa sababu alikuwa anajilipa sasa ndani kwa ndani.

Mwanamuziki Tshala Muana naye alipofanya ziara nchini Tanzania mwanzoni mwa miaka ya 1990, alikuwa akizunguka na bendi ya Zaita Musica iliyokuwa na wanamuziki wa Kitanzania na Kikongomani.

Alipoondoka mwanamama huyo akaenda kurekodi nyimbo mbili za bendi hiyo 'Dezo Dezo' na 'Kokola' ambazo zilitungwa na Ndala Kasheba.

Alichukua bila ridhaa yake, na hata mwisho wa uhai wa Kasheba alifanya kazi kubwa sana ya kufuatilia pesa zake za haki miliki, kwa sababu alishtaki nchini Ufaransa ambapo mwanamama huyo alikwenda kurekodi nyimbo hizo.

Kwa wale wanaoifahamu bendi ya Zaita Musica, ina nyimbo hizo 'Dezo Dezo' na 'Kokola', ambazo zinaimbwa na Kasheba mwenyewe na Tshala Muana naye anazo, yeye aliziiga na kuziboresha zaidi zikipigwa kisasa zaidi, ikichagizwa na ubora wa studio.

Kwa bahati nzuri kesi hiyo ilimalizika vizuri, ingawa Kasheba hakuweka wazi kama alipata pesa au walielewana.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Aka Simtaki-5

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda. Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka. Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**


HIVI mume wangu, kwa nini umeikataa barua ya posa ya Shukuru?" Mzee Chilambo akamtazama mkewe, halafu akamuuliza, "kwani wewe ndiyo unataka kuolewa?"

"Hayo sasa matusi baba Shani, yaani mimi ndiyo nataka kuolewa? Hujanitendea haki, mimi nimeuliza kwa heri tu." "Haya ngoja nikujibu vizuri, kwa sababu ilikuwa ni lazima moja ikataliwe!" Akajibu kwa sauti kubwa iliyomkera mkewe. "Kwa nini mmechukua maamuzi ya mwisho bila hata kuniuliza kwa sababu mimi ndiye ninayeshinda na binti yetu. Yeye anaona nini na anataka nini. Hivi unajua yeye nani anamtaka kati ya hawa wawili?" Akahoji Bi. Hanifa. "Mimi ni mwanaume na ndiyo baba humu ndani, nina maamuzi yangu, tena ndiyo ya mwisho. Nimeamua kuwa simtaki Shukuru. Haiwezekani, mimi ni fukara, halafu binti yangu aolewe na mtu lofa kabisa, yaani afadhali hata mimi nina afadhali." "Kwa nini tusipe uhuru binti yetu achague mchumba anayemtaka?" "Sikiliza mama Shani, isije baadaye sisi ndiyo tukabeba mzigo wa kulea familia, yaani binti ameolewa, badala ya kukaa kwa mumewe, awe hapa na mumewe na watoto tufanye kazi ya kuwatunza sisi, hilo hapana kwa kweli, mimi nimeona mbali, mpaka naamua kijana kutoka kijiji cha Mtapenda ndiyo amuoe binti yetu, mimi na tuliokaa tumefanya upembuzi yakinifu."

"Kwa nini maamuzi ya Shani yasiheshimiwe?" "Hayawezi kuheshimiwa kwa sababu hana akili, anakwenda kumpenda mtu ambaye hana kitu ili yeye mwenyewe apate shida na watoto wake, atupe aibu sisi hapa." Mzee Chilambo aliongea kwa msisitizo.

"Kumbuka kuwa binti yetu ndiye anakwenda kuishi na mwanaume, siyo sisi, kwa nini tusimruhusu aende kuishi na mtu anayempenda kuliko kumlazimisha kama mtumwa?"

"Haiwezekani aolewe na mwanaume fukara kaka yule, sisi tusiwe na pesa, halafu binti yetu aolewe na mtu ambaye ndiyo kabisa afadhali ya sisi. Kwani huyo mwanao hajawaona wanaume wazuri wenye pesa?" Bi. Hanifa akabaki anamwangalia mumewe kwa hasira iliyochanganyikana na huzuni.




**"Kumbuka kuwa binti yetu ndiye anakwenda kuishi na mwanaume, siyo sisi, kwa nini tusimruhusu aende kuishi na mtu anayempenda kuliko kumlazimisha kama mtumwa?"**

"Akae tu hapa, kama kuolewa ataolewa, watakuja wavulana au wanaume wenye uwezo wao, siyo huyu, chawa kwenye nywele, kunguni kwenye nguo hadi funza kwenye miguu."

"Hebu nikuulize babu wewe, kwa nini unamchukia kijana wa watu, kakufanya nini cha zaidi..." Mama Shani akauliza kwa hasira, lakini kabla hajaendelea akajibiwa na mzee Chilambo kwa hasira akiwa amezidisha sauti na kuwa ya juu, kiasi cha mtu kama anapita nje, basi anasikia vizuri tu.

"Amchukie nani kinyangalakata kama kile?" "Ndiyo aliyempenda binti yetu." Nasema mimi sitaki."

"Sasa nani unataka amuoe mwanao? Au unae tayari?" "Halafu mimi ninavyoongea unanijibisha kama mtoto mwenzio kuwa na adabu." Chilambo alimnyooshea mkewe kidole. Hilo alikumtisha Bi Hanifa "Inavyoonekana we bwana pesa inakunoga sana, usiwe na tamaa ya fedha, fedha fedheha." Mzee Chilambo uzalendo ukamshinda, akasimama kutoka kitandani na sura yote ikaielekeza kwa mkewe. "Wewe wewe wewe."

Akaongea kwa hasira. Hasira ambayo ilimfanya kuogopa kidogo, akashusha sauti, ingawa dhamira yake ilikuwa ni ile ile, "Mimi unaniudhi bwana." Akaongea na sauti mdogo kama ya kukata tamaa ambayo ilimfanya mumewe aghairi chochote alichokuwa anataka kukifanya. Hata hivyo bado maneno yaliendelea kumtoka "Naona tayari umeshaanza kunipanda kichwani. Ndivyo ulivyoambiwa kwenu umjibu mumeo hivyo?" Mzee Chilambo alikuwa kwenye kilele cha hasira.

Bi Hanifa aliona muda si mrefu anaweza kuchezea kipigo, akajiondoa taratibu kitandani na kwenda kukaa kwenye mbao kukuu zilizogandana na sponji zilizoonekana wazi. Muunganiko huo zamani uliitwa kochi, lakini kwa sasa haijulikani hata liitwe vipi. Alipewa na mzungu aliyekuwa anamfanyia kazi nyumbani kwake, na alipoondoka akamuachia zawadi mbalimbali, ikiwemo kochi ambalo kwa sasa limekuwa kuukuu.

"Hii tabia umeianza lini?" Akauliza mzee Chilambo huku akimgeukia mkewe kule alikokuwa amekaa. "Unataka kunitawala eee, hii namba nyingine, kimya na nisikusikie tena unanijibu." Mama Shani alishamfahamu mumewe akiwa kwenye kilele cha hasira. Miaka 30 ya ndoa siyo mchezo. Alibaki kimya akijua sauti yoyote itakayotoka mdomoni mwake, itamsababishia matatizo.

******************************

"Tumeamua kurudisha barua moja na kuipitisha moja." Mzee Chilambo alimwambia Shani aliyekuwa amekaa kwenye mkeka, pembeni akiwa mtu mmoja ambaye hamwelewi vizuri aliyekaa kwenye kigoda, pamoja na mama yake alikaa naye mkekani upande wa kushoto. Mwenyewe mzee Chilambo alikuwa ameketi kwenye kiti chake cha uvivu.

Ilikuwa ni wiki moja tangu Shani arejee kutoka kwa shangazi yake ambako akikaa huku kwa wiki mbili kupisha mchakato wa kujibiwa barua mbili za posa zilizowasilishwa kwao. Walikuwa ni washenga wawili kwa nyakati tofauti walioleta posa kwa ajili yake.

Wazazi wakaona haifai mchakato ufanyike binti awepo, wakaamua kumkimbizia kwa shangazi yake.

Baada ya kufanyika, alirejeshwa na leo anapewa mrejesho ya kile kilichofanyika.

"Sasa tunakuuliza uko tayari kuolewa?" akamuuliza mtoto wake. "Imetoka kwa nani?" Shani akauliza. Jibu hilo lilionekana kumkera baba yake. Mshenga aliona hiyo hali akasema, msimfiche mtoto tafadhali mwambieni ukweli." Mzee Chilambo akakohoa kidogo, halafu akaonekana kama kukaa vizuri hivi na kumwambia. "Imetoka kwa mzee Kandege." Jibu hilo lilionekana kumshangaza Shani. Katika kumbukumbu zake hajawahi kulisikia jina hilo kwenye kijiji chao. Na wala mpenzi wake Shukuru hakuna na ubini huo, labda ya babu yake. "Kandege?" Akahoji. "Ndiyo ni mzee kutoka kijiji cha jirani, Mtapenda, huyo mzee ana kijana wake anaitwa Fotu, ndiyo anataka kukuoa na yeye ndiye aliyefuzu vigezo vya kukuoa."

Maneno hayo yalimchanganya Shani. Alichojua ni kwamba mama yake angefikisha ujumbe kwa waliokuwa wanachuja hizo barua mbili na kubaki ya yule anayependa tu. "Hapana baba." Akajibu lakini kwa sauti ya chini ya woga. "Unasemaje?" Baba akahoji. "Baba nadhani barua ambayo ningependa ikubaliwe ni ile mliyoiacha." Macho yalimtoka pima mzee Chilambo. Alionekana kuwa na hasira ambazo zilimfanya ashindwe kuongea. "Mwanangu, kwa nini unakataa bahati hii?" Bi Hanifa alionekana kusikitika. Shani akaonekana kumshangaa mama yake. Alionekana kubadilika. Awali alionekana kama yupo naye na akamkabidhi kazi ya kuwashawishi barua anayoitaka ipitishwe. Aliona amesalitiwa. Na hilo lilionekana kumsikitisha sana. Asichokijua ni kwamba mama yake alifanya kila njia lakini ikashindikana. Ilikuwa nusura achezee kichapo kutoka kwa mumewe. Siku tatu baadaye akaletewa pesa kiasi cha shilingi elfu kumi ambacho hakikuwa kwenye mahesabu yoyote wa posa wala nini. Akaona bure awe upande huo huo. Ukinshindwa adui yako ni bora kuungana naye. Ndivyo alivyoona. "Unasikia, ukoo ambao unataka kumuoa una uwezo mkubwa, hii barua tu imewekwa elfu thelathini, ulione wapi hii, usiipoteze binti." Mshenga akasaidia. "Nimesema 'aka huyo mchumba simtaki."

**ITAENDELEA JUMAPILI**





# SHUSHO AKUMBANA NA BARIDI KALI NAIROBI

MWIMBAJI wa muziki wa Injili, Christina Shusho ametua nchini Kenya na kukumbana na hali ya baridi kali ambayo kwake imekuwa na tatizo kuzoea.

Baada ya kutua jijini Nairobi, Shusho alipigwa na butwaa baada ya kukuta hali ya hewa kuwa ya baridi tofauti na Dare Es Salaam, jambo lilionekana kumshtua na kuuliza kwa nini hakuelezwa hiyo mapema.

Msanii huyo alilalamika kwamba Jiji la Nairobi lilikuwa na baridi kali kuliko Tanzania, lakini alisema hali hiyo itahamasisha watu kwenda kuhudhuria katika tamasha ambalo yeye atatumbuiza.



# CARD B ATARAJIA MTOTO KWA BABA ANAYEMKATAA

RAPA mkali kutoka Marekani, Cardi B, ametangaza yuko katika siku za mwisho kumpata mtoto wake wa tatu na mume wake Offset.

Cardi B aliwafahamisha mashabaiki wake baada ya kuonekana amevaa mavazi yanayoonyesha ujauzito wake.

Mwanamuziki huyo tayari amefungua kesi ya talaka dhidi ya Offset, huku akieleza hatua hiyo haitegemei na hali aliyokuwa nayo kwa sababu suala hilo halitamuhusu mtoto atakayezaliwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BAYERN YAIKATALIA MAN UNITED

KLABU ya Bayern Munich imekataa dau la Manchester United mara mbili kwa mlinzi wa kati wa Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 24, na beki wa Morocco, Noussair Mazraoui mwenye umri wa miaka 26. (**Telegraph**)

### GORDON KUPEWA MKATABA MPYA

NEWCASTLE United inapanga kuanzisha mazungumzo kuhusu mkataba mpya na winga wa England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 23, atakaporejea kutoka mapumzikoni baada ya mashindano ya Euro 2024. (**Athletic**)

### RODRIGUEZ ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham ipo katika mpango wa kumsajili kiungo wa Argentina, Guido Rodriguez mwenye umri wa miaka 30, kama mchezaji huru baada ya kuondoka Real Betis. (**Standard**)

### PHILLIPS ANATAKA MKATABA

KIUNGO wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, ameiambia Manchester City kuwa anataka uhamisho wa kudumu kutoka kwa klabu hiyo, huku Everton na Aston Villa zikizingatia mkataba wa mkopo. (**Football Insider**)

### IHENACHO KUTUA SEVILLA

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Kelechi Iheanacho mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kujiunga na Sevilla baada ya mkataba wake na Leicester City kumalizika. (**Sky Germany**)

### WILLIAMS AWANIWA PSG

KLABU ya Paris St-German bado ina nia ya kumsajili winga wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22. (**RMC**)

### RAPHINHA ATAKIWA VILLA

ASTON Villa inataka kumnunua mshambuliaji wa Barcelona na Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 27, msimu huu. (**Football Insider**)

### GYOKERES AGOMBEWA EPL

KLABU za Liverpool na Tottenham Hotspur zimeungana na Arsenal katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 26 kutoka Sporting Lisbon. (**Football Insider**)

### ARSENAL, CHELSEA VITANI

ARSENAL na Chelsea ziko tayari kuwania saini ya mshambuliaji wa Manchester City na Argentina, Julian Alvarez mwenye umri wa miaka 24. (**TeamTalk**)

### FELIX, ASTON VILLA HAKIJAELEWEKA


MKATABA kati ya Aston Villa na Atletico Madrid kumuhusu mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 24, haujakamilika bila pendekezo rasmi lililotumwa kwa klabu hiyo ya Hispania. (**Fabrizio Romano**)

### N'CASTLE KUKAMULIWA KWA THIAW

KLABU ya Newcastle italazimika kulipa euro milioni 40 kama wanataka kumsajili beki wa kati Mjerumani, Malick Thiaw mwenye umri wa miaka 22 kutoka AC Milan. (**Gazzetta dello Sport**)



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



## CHELSEA YAMWONYA GALLAGHER

**LONDON,** England

**Yamchimba mkwara hatoruhusiwa kujiunga na timu hiyo endapo atakataa dili la...**

CHELSEA imemwambia Conor Gallagher kuwa huenda hataruhusiwa kurejea kwenye kikosi cha kwanza iwapo atakataa kuhamia Atletico Madrid, kwa mujibu wa ripoti.

The Blues wamekubali ofa ya kiungo huyo kutoka Atletico katika siku za hivi karibuni inayoaminika kuwa na thamani ya pauni milioni 33.8, ingawa bado hajakubali maslahi binafsi na timu hiyo ya Hispania.

**Ripoti pia zimesema kuwa Gallagher tayari amekataa ofa mbili za mkataba mpya kutoka kwa Chelsea, ingawa pendekezo lao la hivi punde bado liko mezani.**

Ripoti ya 'The Times' imesema Chelsea sasa imemwonya Gallagher kwamba anaweza kukabiliwa na rungu la 'kufukuzwa' kutoka kikosi cha kwanza na kituo chao cha mazoezi cha Cobham ikiwa hatasaini Atletico au kukubali ofa ya mwisho ya klabu ya mkataba mpya.

Mbali na ofa ya Atletico, Chelsea wanatarajia Tottenham Hotspur kuwasilisha ombi la kumsajili katika siku zijazo.

Spurs wamekuwa na nia ya muda mrefu ya kumnunua Gallagher lakini walishindwa katika jaribio la kumsajili majira ya joto mwaka jana alipotolewa kwa mara ya kwanza kwa uhamisho.

Hata hivyo, ripoti hiyo inaongeza kuwa Spurs wanampa kipaumbele fowadi mpya na hakuna uwezekano wa kumnunua Gallagher hadi mwisho wa dirisha.

Mkataba wa sasa wa Gallagher huko Stamford Bridge unamalizika mwaka 2025, hivyo basi klabu hiyo inataka kupanga mustakabali wake kabla ya mwisho wa mwezi huu.

# ÁLVAREZ KUAMUA HATIMA YAKE MANCHESTER CITY



**MADRID,** Hispania

KLABU ya Atlético Madrid inazidi kuwa na matumaini juu ya uwezekano wa kumsajili fowadi wa Manchester City, Julián Álvarez kama sehemu muhimu ya kikosi kilichoboreshwa cha kocha Diego Simeone, kwa mujibu wa ESPN.

Na sasa Atletico imefanya mazungumzo na wawakilishi wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina na wana imani kwamba ana nia ya kujiunga na klabu hiyo, vyanzo vilisema, jambo ambalo litafanya mazungumzo na Man City kuwa rahisi.

Makubaliano ya mchezaji huyo ambaye usajili wake unaonekana kuwa kipaumbele, yatajumuisha misimu mitano na ada ambayo inaweza kufikia Euro milioni 60 ikiwa Man City itakubali kuelekea kwenye meza ya mazungumzo.

Álvarez alicheza kwa dakika 90 siku ya Ijumaa wakati Argentina wakifungwa bao 1-0 dhidi ya Ufaransa katika robo fainali kwenye Michezo ya Olimpiki jijini Paris.

Baada ya mechi, aliulizwa kuhusu mustakabali wa klabu yake: "Nilizingatia michuano hii. Tutaona nini kitatokea na maisha yangu ya baadaye. Sasa nachukua mapumziko ya siku chache kisha nitaamua," alisema Álvarez.

Msimamo wa Man City unabaki kuwa mlango uko wazi kwa mchezaji wao yeyote kuondoka iwapo tathmini ya klabu itatimizwa.

Wakati huo huo, wawakilishi wa Álvarez wanasita kuzungumzia waziwazi uwezekano wa kuhamia Atletico na wanasubiri hadi baada ya Olimpiki kuzungumza na City kuhusu mipango yao ya fowadi huyo.

Hata hivyo, chanzo kimoja kilisema kwamba hadhi ya Erling Haaland kama mshambuliaji chaguo la kwanza la City inachanganya uhakikisho wowote wa muda wa kucheza ambao klabu inaweza kumpa Álvarez.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Álvarez anataka kuchukua hatua inayofuata kuelekea kuwa mwanzilishi, ambayo Atlético inaweza kumuhakikishia chini ya Simeone.

Baada ya kuondoka kwa Álvaro Morata na Memphis Depay, Atletico wamekuwa kwenye mazungumzo na Villarreal kwa ajili ya Alexander Sørloth, ingawa watahitaji fowadi mwingine kukidhi mahitaji yao.

## Giroud: Zlatan alinishauri kuhamia Marekani


**LOS ANGELES,** Marekani

WAKATI klabu ya LAFC ya Ligi Kuu ya Soka ya Marekani ilipomtambulisha rasmi nyota wao mpya, Olivier Giroud siku ya Alhamisi, mshambuliaji huyo wa Ufaransa alifichua kwamba alifanya uamuzi wake kutua MLS kwa sababu ya ushauri wa Zlatan Ibrahimovic.

"Nilizungumza na Zlatan ambaye alikuwa hapa," alisema Giroud kuhusu nyota wa zamani wa Manchester United, Inter Milan na Paris Saint-Germain, ambaye alicheza misimu ya 2018 na 2019 kwa LA Galaxy.

"Aliniambia nitafurahia, ni ligi ya washambuliaji, timu ambazo hawachezi kuweka matokeo au kulinda. Wanacheza kufunga mabao na kuwapa raha mashabiki wenye hamasa."

Mmoja wa nyota wa kizazi chake waliofanikiwa zaidi, Giroud ameshinda mataji 11 makubwa na kufunga karibu mabao 300 huku akicheza zaidi ya michezo 700 katika ngazi ya klabu.



Mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 37 alisaini na LAFC mwezi Mei.

Giroud amekuja Marekani baada ya miaka 18 katika ligi kuu za kulipwa katika Ligue 1, Premier League na Serie A, iliyojumuisha misimu minne iliyopita akiwa na AC Milan. Ana mabao 285 katika mechi 716 za klabu.

"Ninaweza kuleta uzoefu wangu, taaluma yangu, malengo yangu, na bila shaka ushauri wote ninaoweza kutoa," alisema. "Nitapatikana kwa washirika wangu. Ni michuano tofauti kulinganisha na Ulaya ambayo iliimarika zaidi miaka michache iliyopita.

# Man United yakomaa na De Ligt, Mazraoui



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeongeza juhudi za kuimarisha safu yao ya ulinzi kwa kutoa ofa kwa wachezaji wawili wa Bayern Munich, Matthijs de Ligt na Noussair Mazraoui, kwa mujibu wa ESPN.

De Ligt na Mazraoui wanapatikana msimu huu wa majira ya joto huku Bayern wakiwathaminisha wawili hao kwa jumla ya pauni milioni 55.

Dau la United limeshuka chini ya thamani hiyo na linatarajiwa kukataliwa na timu hiyo ya Bundesliga.

Kocha Erik ten Hag anataka kuongeza beki mwingine wa kati na beki wa pembeni kwenye kikosi chake kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili.

Leny Yoro, aliyesajiliwa kwa kiwango cha pauni milioni 52 kutoka Lille, amekuwa nje kwa miezi mitatu kutokana na kuvunjika mguu huku beki wa kushoto Tyrell Malacia hatarajiwi kurejea kwa miezi miwili zaidi huku akiendelea kurejea kutokana na jeraha la goti.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba mpango wa United ulikuwa kila wakati kutafuta nyongeza zaidi za ulinzi na mawasiliano rasmi na Bayern hayajachochewa na jeraha la Yoro.

Bado kuna nia ya kumtaka Jarrad Branthwaite, ambaye anaweza kucheza katika nafasi ya beki wa kati na beki wa kushoto, ingawa hitaji la Everton la zaidi ya pauni milioni 70 inaonekana kuwa tatizo.

United tayari wameona ofa zao mbili zimekataliwa na Everton.

Licha ya kutumia zaidi ya pauni milioni 85 kuwanunua Yoro na mshambuliaji Joshua Zirkzee msimu huu wa majira ya joto, United wameweza kuwasilisha ofa muhimu kwa Bayern kwa sababu ya imani inayoongezeka kwamba Aaron Wan-Bissaka atakamilisha uhamisho wa kwenda West Ham.

United inamtathimini beki huyo wa kulia kati ya pauni milioni 15 hadi 20 na makubaliano na West Ham yanakaribia.

West Ham walikuwa wameonesha nia ya kumnunua Mazraoui kabla ya dili hilo kuvunjika.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba De Ligt na Mazraoui wana nia ya kuhamia Old Trafford ikiwa klabu hizo mbili zinaweza kukubaliana.

## HABARI MICHEZO

# COASTAL UNION YAFUATA MAKALI KISIWANI PEMBA

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Coastal Union kimehamisha kambi yake kutoka Unguja na kuelekea Pemba kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wao wa Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC utakaochezwa Agosti 8 kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Abbas El Sabri alisema wanahamisha kambi hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo.

"Leo (jana) tumehamishia kambi yetu Pemba kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu huo ambao unatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa, lengo ni kupata ushindi na kusonga mbele kuingia kwenye fainali," alisema El Sabri.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, David Ouma, alisema michezo minne ya kirafiki waliyoicheza visiwani humo imemsaidia kutengeneza muunganiko wa timu na kutoa taswira halisi pindi msimu ujao utakapokuwa tumeanza.

Alisema malengo yake ni kushinda kwenye mchezo huo wa Ngao ya Jamii na anashukuru mpaka sasa hana mchezaji yeyote ambaye ni majeruhi.

"Michezo ya kirafiki tuliyoicheza imenisaidia kuimarisha zaidi kikosi changu ambacho ninaamini kitafanya vizuri katika mchezo huo pamoja na ile ya msimu ujao wa Ligi Kuu itakayoanza Agosti 16, mwaka huu," alisema Ouma.

Mpaka sasa timu hiyo imecheza michezo minne ya kirafiki ambapo mchezo wa kwanza walicheza na Tekeleza FC na kufanikiwa kushinda bao 1-0, mchezo wa pili walicheza na Kombaini na kushinda mabao 8-0, pia walicheza na Jamhuri na kufanikiwa kuichapa mabao 4-0 kabla ya kucheza na Chipukizi na kuibuka na ushindi wa mabao 4-0.




Baadhi ya makocha na wachezaji wa nchi zinazoshiriki mashindano ya Kriketi ya ICC daraja la pili wakiwa pamoja katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kagera Sugar kutangaza 'vyuma' vyake

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar imesema wakati wowote kuanzia kesho itaanza kutangaza wachezaji wake wapya iliyowasajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kaimu Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Stephen Julius, amesema wataanza kuwaweka hadharani wachezaji wao wapya ambao anaamini wataifanyia makubwa klabu hiyo.

Alisema hayo baada ya mashabiki wa timu hiyo kulalamikia ukimya wa timu hiyo, huku baadhi ya klabu hata zile zilizopanda daraja msimu huu zikitangaza usajili wao.

Aliwaambia mashabiki wa timu hiyo kuwa ukimya huo siyo kama hawajasajili, bali wameshafanya hivyo na tayari wapo kambini wakifanya mazoezi ya mwanzo wa msimu, kilichobaki ni kuwatambulisha tu.

"Tulikuwa na mambo mengi, kwanza tulianza kikao na wazee wa mkoa, baadaye watakuja mashabiki, lakini tupo katika hatua za mwisho kabisa za kutangaza wachezaji wapya, wiki hii tunawaweka hadharani wote waliosajiliwa kuelekea msimu ujao.

Siyo kama hatujasajili, tumeshusha vyuma, wachezaji wapo kambini wanaendelea na maandalizi wadau wa soka wakae mkao wa kula," alisema Stephen.

Timu hiyo imekuwa ikifanya mazoezi ya utimamu wa mwili kwenye fukwe za Ziwa Victoria nyakati za asubuhi na jioni ikifanya maandalizi Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera.

Mashabiki wameonekana kuwa na wasiwasi na ukimya huo, baada ya timu hiyo kupoteza baadhi ya wachezaji wake muhimu baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu msimu uliopita.

Wachezaji hao ni Ally Nassor 'Ufudu', aliyetimkia Mashujaa FC, Allain Ngeleka, kipa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo aliyesajiliwa na Dodoma Jiji, Mbaraka Yusuph aliyejiunga na Coastal Union, Mubarack Amza ambaye kwa sasa ni mali ya Namungo FC.

## Gamondi awaita mashabiki kwa Mkapa leo

INATOKA UK. 24

inawezekana kuna vitu vikaongezeka zaidi kwa sababu tumefanya vyema msimu uliopita," alisema Gamondi.

Alisema katika mechi ya leo atajitahidi kuchezesha wachezaji wengi, kila mchezaji apate dakika kadhaa ya kucheza.

"Siyo kama naidharau Red Arrows, ni timu nzuri, najua na wao wamekuja kupambana, lakini ukweli unabaki pale pale leo ni burudani zaidi kuliko ushindani, ingawa hii haiwezi kutufanya tusitafute ushindi kwa ajili ya furaha ya mashabiki wetu," alisema.

Yanga inakwenda kucheza dhidi ya Red Arrows, ambayo hivi karibuni ilitwaa Ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati, maarufu kama 'Kagame Cup', michuano ilifanyika nchini Tanzania kwenye viwanja vya KMC, Mwenge na Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.


Tamasha la leo litakuwa la sita kufanywa na klabu hiyo, ambapo kwa mara ya kwanza lilifanyika mwaka 2019 ikicheza dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya na kutoka sare ya bao 1-1.

Lilifanyika kwa mara ya kwanza miaka 10 baada ya klabu ya Simba kuasisi tamasha la 'Simba Day' mwaka 2009.


Kama lilivyokuwa kwa watani wao jana, tamasha hilo litaanza asubuhi, ambapo kutakuwa na burudani mbalimbali kutoka kwa wasanii na bendi za muziki wa dansi, kabla ya michezo kadhaa ya mpira wa miguu kuanza na baadaye kuanza kutambulisha wachezaji wa zamani na wapya waliosajiliwa kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano na litahitimishwa kwa mchezo huo wa kirafiki.

Wanachama na mashabiki wa Yanga kwa mara ya kwanza watashuhudia wachezaji wao wapya waliosajiliwa, wakicheza katika ardhi ya Tanzania baada ya kushuhudia kwenye runinga nchini Afrika Kusini.

Baadhi ya wachezaji hao ni Clatous Chama aliyetoka Simba, Prince Dube aliyesajiliwa kutoka Azam FC, Duke Abuya kutoka Singida Black Stars, Aziz Andambwile, akitokea Singida Fountain Gate.



Michezo
Jumapili Agosti 4, 2024
Nipashe



**Chelsea yamwonya Gallagher** UK. 21



Baadhi ya mashabiki wa klabu ya Simba wakiwa ndani ya Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye kilele cha Tamasha la 'Simba Day' jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waarabu kumng'oa Onana Simba SC

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Watuma ofa nono, viongozi waridhia kumwachia huku wakisitisha mpango wa...

WAKATI jana wakihitimisha kwa mafanikio tamasha la kila mwaka la 'Simba Day' lililofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, klabu ya Simba inajiandaa kumpiga bei winga wake, Onana, imefahamika.

**Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema klabu ya Muaither ya nchini Qatar imetuma ofa ya Dola za kimarekani 100,000 kama ada ya uhamisho na pesa kama hizo pia ikiwa ni ya mchezaji mwenyewe kwa ajili ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo.**

Taarifa zinasema Onana hakuwa mmoja wa wachezaji waliofanya mazoezi na kikosi hicho kuelekea katika mechi ya tamasha la Simba Day jana.

"Ni kweli ipo hiyo ofa, na wala viongozi hawana tatizo na hilo kwa sababu kama utakumbuka alichelewa kujiunga na kambi kwa kuwa kulikuwa na mpango wa kuvunja naye mkataba lakini kufeli kwa dili ya Elie Mpanzu kukamwokoa. Ila sasa usajili wa Moussa Kamara nao umechangia kuuzwa kwa sababu inaonekana hakuna uwezekano wa kumkata Ayoub Lakred ambaye ameumia na atakaa nje kwa muda wa wiki sita," alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo.

Alisema awali Simba ilitaka kuliondoa jina la Ayoub Lakred kwenye orodha ya wachezaji 12 wa kigeni ili liingizwe la Kamara lakini dili la Onana limesababisha mpango huo kusitishwa.

"Kwa maana hiyo Simba itakuwa na makipa wawili wa kigeni msimu ujao, na imelazimika kufanya hivyo kwa sababu Ayoub atakaa nje wiki sita sawa na mwezi mzima, lakini ameongezeka uzito, hivyo akipona ana kazi nyingine ya kupunguza uzito, hiyo ni miezi miwili wakati timu inakabiliwa na michezo muhimu mwanzoni tu mwa msimu," alisema mtoa taarifa.

Kabla ya klabu hiyo kuleta ofa, Onana anayecheza nafasi ya winga wa kushoto, alikuwa anatakiwa na klabu za Kaizer Chiefs, Orlando Pirates za Afrika Kusini na Wydad Casablanca ya Morocco.

Mchezaji huyo raia wa Cameroon, alisajiliwa na klabu hiyo mwanzoni mwa msimu uliopita akitokea klabu ya Rayon Sport ya Rwanda.

Onana akiondoka Simba ataungana na nyota wengine, Clatous Chama, Henock Inonga, Sadio Kanoute na Saido Ntibazonkiza kuachana na timu hiyo.



## Gamondi awaita mashabiki kwa Mkapa leo

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwenda kwa wingi leo, Uwanja wa Benjamin Mkapa, kushuhudia soka safi litakalochezwa na vijana wake dhidi ya Red Arrows kutoka Zambia katika Kilele cha Wiki ya Mwananchi.

Gamondi amesema mchezo wa leo sio wa kusaka pointi wala ushindi kwa ajili ya kombe lolote, hivyo anataka wachezaji wake wafurahie soka, na ushindi utakuja kama wakitandaza soka safi ambalo anataka wacheze.

"Ni Siku ya Mwananchi, najua kutakuwa na watu wengi uwanjani, kutafurika mashabiki, najua hili kwa sababu msimu uliopita nilishuhudia pale, lilikuwa ni moja kati ya tukio langu bora sana kuliona, naamini safari hii itakuwa hivyo hivyo, ingawa pia nadhani

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042